Maelezo ya

# Nyakati saba za kanisa

## Sura ya Nne

## The Smyrnaean Church Age

Ufunuo 2:8-11

*"Na kwa malaika wa kanisa lililoko Smirna andika; Haya ndiyo anenayo Yeye aliye wa Kwanza na wa Mwisho, Aliyekuwa amekufa, kisha akawa hai;*

*Nayajua matendo yako, na dhiki yako, na umaskini wako, (lakini, u tajiri), na najua na matukano ya hao wasemao ya kuwa ni Wayahudi, nao sio, bali ni sinagogi la Shetani.*

*Usiogope mambo yatakayokupata: tazama, huyo ibilisi atawatupa baadhi yenu gerezani, ili mjaribiwe, nanyi mtakuwa na dhiki siku kumi: Uwe mwaminifu hata kufa, nami nitakupa taji ya uzima.*

*Yeye aliye na sikio, na alisikie Neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa; yeye ashindaye hatapatikana na madhara ya mauti ya pili."*

**UTANGULIZI**

Ili kuburudisha nia zenu nataka kuonyesha tena jinsi tunavyoweza kupata majina ya wale wajumbe wa nyakati mbalimbali. Mungu katika mapenzi Yake makamilifu amehakikisha ya kwamba historia ya kanisa la Agano Jipya haikupotea, kama vile alivyohakikisha ya kwamba historia ya Israeli haingepotea kwa kuiweka katika Biblia na kuithibitisha leo kwa wingi wa magombo, vyombo vya udongo na kazi nyingine sanaa ambazo wataalamu wa kuchimbua mambo ya kale wamevumbua na kutafsiri. Kwa kweli tuna ufafanuzi wa historia ya Biblia tangu ukurasa wa kwanza hadi sasa.

Kwa hiyo kwa kusoma historia tunaweza kuona ni mtu gani ama ni watu gani katika nyakati mbalimbali waliokuwa karibu sana na kile kielelezo cha asili cha Mungu, Mtume Paulo. Wale ambao Mungu aliwatumia kuwarudisha watu Wake kwenye Neno la Kweli wangekuwa ndio tungeangalia. Ndipo kutokana na hao kungekuweko na mmoja kwa kila wakati ambaye angejitokeza dhahiri kuliko wote kama aliye karibu sana katika kielelezo cha Neno na nguvu. Huyo angekuwa mjumbe. Zile nyakati pia zinapatikana kwa kusoma historia. Mtu anapaswa tu kusoma zile nyakati kama zinavyoonekana katika Ufunuo na yote yanaendana kikamilifu na historia jinsi ZIPASWAVYO HASA KULINGANA. Kwa kuwa nyakati za kanisa zilitabiriwa na Mungu na tabia zake halisi zikafunuliwa, basi sharti, historia ambayo ingefuata ingekuwa kama vile inavyoelezewa na Biblia. Ni rahisi—lakini basi urahisi ni ufunguo wa Neno. Sasa pamoja na haya yote sijawa tu mwanafuzi na mwanahistoria, nimejitahidi kuwa mtu wa kiroho, nami ilikuwa tu ni kwamba nimewachagua watu hawa kwa kibali dhahiri tu cha Roho wa Mungu. Hii ni kweli kama Mungu anavyoujua moyo wangu.

**MJUMBE**

Tukitumia kanuni tuliyopewa na Mungu ya kumchagua mjumbe kwa kila wakati, sisi bila kusitasita tunatangaza ya kwamba Ireneo aliinuliwa na Bwana kwenye nafasi hiyo. Yeye alikuwa mwanafunzi wa yule mtakatifu mkuu na shujaa wa imani, Polikapu. Na hapana shaka alipoketi miguuni pa mtu huyo mashuhuri alijifunza neema za Kikristo zilizotiririka kutoka katika maisha yake yaliyowekwa wakfu, kwa kuwa Polikapu alikuwa mmoja wa watakatifu maarufu kweli wa nyakati zote katika mtazamo wa maisha yasiyo na lawama.

Utakumbuka kutokana na kusoma kwako binafsi ya kwamba Polikapu alifia imani yake. Akiwa mzee sana asiweze kukimbia, na akiwa mtu mwaminifu sana hangeweza kumruhusu mwingine kumficha na halafu aadhibiwe kwa kufanya jambo hilo, yeye alijitolea apate kufa. Lakini kabla hajauawa, aliomba na akapewa ruhusa ya kuwaombea ndugu zake katika Bwana kwa muda wa masaa mawili, kumwombea liwali, adui zake na waliomkamata. Kama wale watakatifu mashuhuri wa nyakati zote, na huku akitaka ufufuo bora, alisimama imara, akikataa kumkana Bwana, na akafa akiwa na dhamiri safi. Alifungiwa kwenye mti wa kuchomea watu moto (akiwa hajafungwa kwa kuwa aliwaomba wasimfunge) kisha moto ukawashwa. Moto ukainama mbali na mwili wake, ukikataa kumgusa. Kisha akachomwa kwa upanga. Wakati hili lilipofanywa, maji yakatiririka kutoka ubavuni mwake ukaizima ile miali ya moto. Roho yake ilionekana dhahiri ikiondoka katika mfano wa hua mweupe aliyetoka kifuani mwake. Hata hivyo pamoja na ushuhuda huu mkuu, mwanafunzi huyu wa Yohana Mfunuzi hakuupiga vita ule utaratibu wa Unikolai, kwa maana yeye mwenyewe aliegemea kwenye madhehebu, bila kutambua ya kwamba ile shauku ya ushirika na kile kilichoonekana kama mpango mzuri wa kusaidia kazi ya Mungu ilikuwa kweli ni ujanja wa yule adui.

Kwa Ireneo haikuwa hivyo. Yeye alipinga kila aina ya madhehebu. Pia, historia yake ya maisha,

ambamo alimtumikia Bwana, ilikuwa moja ya dhihirisho kubwa katika Roho Mtakatifu; na Neno lilifundishwa kwa uwazi usio wa kawaida na kulingana na kanuni zake za asili. Makanisa yake kule Ufaransa yalijulikana kwamba yalikuwa na karama za Roho kati yao, kwa maana watakatifu walinena kwa lugha, walitabiri, walifufua wafu, na waliponya wagonjwa kwa maombi ya imani. Aliona hatari ya shirika la undugu wa aina yo yote kati ya wazee, wachungaji nk. Yeye alisimama imara kuunga mkono kanisa la mtaa fulani lililokuwa na nia moja, lililojazwa na Roho, na linalodhihirisha karama. Naye Mungu alimheshimu kwa nguvu za Mungu zilizodhihirishwa miongoni mwa watakatifu.

Pia alikuwa wazi juu ya ufahamu wake wa Uungu. Na kwa kuwa alikuwa mwanafunzi wa Polikapu, ambaye naye alikuwa mwanafunzi wa Yohana Mtakatifu, tunaweza kujua kwa uhakika ya kwamba alikuwa na fundisho kamilifu iwezekanavyo juu ya somo hili. Katika Kitabu cha 1, ukurasa wa 412 cha Waanzilishi Waliotangulia Nikea tuna tamshi lake hili juu ya Uungu. “Misemo mingine yote, vivyo hivyo, inaeleza sifa za mmoja, na mtu yule yule, Bwana wa Uweza, Bwana, Baba wa Wote, Mungu Mwenyezi, Aliye Juu, Muumba, Mwenye Kubuni, na kadhalika, haya si majina na sifa za wenye uhai mbalimbali wanaofuatana, bali ni ya mmoja na yeye yule.” Yeye alionyesha waziwazi ya kwamba hizi si kitu bali ni sifa kama vile katika Ua la Uwandani, Nyota Yenye Kung'aa ya Asubuhi, Aliye Mzuri Kuliko Elfu Kumi, nk. Wala hakuna ila Mungu MMOJA. Jina Lake ni Bwana Yesu Kristo.

Kwa hiyo kushikilia kwake Neno kwa dhati, ufahamu wake mzuri sana wa Maandiko, na nguvu za Mungu zilizofuatana na huduma hiyo, yeye ndilo chaguo sahihi kwa ajili ya wakati huo. Ni huzuni kabisa kwamba zile nyakati nyingine hazikuwa na mizani kama hiyo ya tunda, nguvu, na uongozi katika Roho Mtakatifu na Neno, katika wajumbe wao.

**SMIRNA**

Mji wa Smirna ulikuwa kaskazini kidogo ya Efeso kwenye mlango wa Ghuba ya Smirna. Kwa sababu ya bandari yake nzuri sana ilikuwa ni kituo cha biashara mashuhuri kwa mauzo yake ya nje. Pia ulisifika sana kwa shule zake za ufasaha wa kuongea, falsafa, udaktari, sayansi, na majengo mazuri. Wayahudi wengi waliishi kule, nao waliupinga sana Ukristo, hata zaidi kuliko Warumi. Kwa kweli, Polikapu, askofu wa kwanza wa Smirna aliuawa na Wayahudi kwa ajili ya imani yake na inasemekana ya kwamba Wayahudi hao waliinajisi siku yao takatifu (Jumamosi) kubeba kuni za kuteketezea maiti yake.

Neno Smirna linamaanisha, “uchungu,” likitokana na neno, manemane. Manename ilitumiwa katika kuhifadhi maiti. Kwa hiyo tuna maana mbili zinazopatikana katika jina la wakati huu. Ulikuwa ni wakati wa uchungu uliojaa mauti. Ile mizabibu miwili katika utaratibu wa kanisa ilikuwa ikitengana zaidi na zaidi huku uchungu dhidi ya mzabibu wa kweli unaongezeka upande wa ule wa uongo. Mauti hayakuwa tu ndiyo mbegu ya huo mzabibu wa uongo bali hata katika ule mzabibu wa kweli kulikuwako na kupooza kulikokuwa kunanyemelea kisiri na pia udhaifu kwa sababu walikuwa tayari wameondoka kwenye kweli isiyoghoshiwa ya miaka michache ya kwanza baada ya Pentekoste; wala hakuna mwamini wa kweli aliye na nguvu zaidi na afya kiroho na mzima kuliko kujua kwake na kushikilia kwake Neno halisi la Mungu, kama inavyoonekana kwa mifano mingi sana katika Agano la Kale. Madhehebu yalikuwa yakikua haraka, yakithibitisha na kuongezea kufa kwa wafuasi wake, kwa kuwa uongozi wa Roho Mtakatifu uliondolewa na badala yake kanuni za imani, mafundisho ya sharti na kawaida za dini zikachukua nafasi ya Neno.

Wakati Israeli walipoingia katika muungano usio halali na ulimwengu, na kuunda ushirika kwa ndoa, siku ilifika hatimaye wakati ulimwengu ulipotawala na Babeli ikawachukua watu wa Mungu utumwani. Sasa wakati walipokwenda utumwani waliingia wakiwa na ukuhani, hekalu na Neno. Lakini waliporudi walikuwa na marabi, utaratibu wa kitheolojia wa Mafarisayo, sinagogi, na Kitabu cha Dini ya Kiyahudi. Na wakati Yesu alipokuja walikuwa wamepotoka sana hivi kwamba aliwaita wa baba yao, ibilisi, akawaita hivyo ingawa walikuwa wa ukoo wa Ibrahimu kimwili. Katika wakati huu tunaona jambo lile lile likitukia. Hata hivyo, kama vile, 'Israeli wote' si Israeli, ila kundi dogo lilikuwa ndilo Israeli wa kweli wa Kiroho, kwa hiyo daima kutakuwa na kundi dogo la Wakristo wa kweli, bibi-arusi wa Kristo, mpaka alipokuja kwa walio Wake.

Katika mji huu kulikuwa na mahekalu mawili mashuhuri. Moja lilikuwa ni hekalu lililojengwa kwa ajili ya ibada za Zeusi, na hilo lingine alijengewa Sebele. Na kati ya mahekalu haya mawili kulikuwa na barabara nzuri sana ya nyakati za kale, inayoitwa Barabara ya Dhahabu. Kwangu mimi hii inaonyesha kupenyeza zaidi kwa upagani ambao tayari ulikuwa umeanza katika wakati wa kwanza, lakini ulijulikana kuwepo huko Rumi tu. Kule kuunganishwa kwa mahekalu hayo mawili ya mungu wa kiume na mungu wa kike ni mbegu ya ibada za Mariamu ambapo Mariamu anaitwa mama wa Mungu na anapokea heshima na sifa na nguvu zikimpa usawa na Yesu Kristo.

Ile Barabara ya Dhahabu inayoziunganisha ni picha ya tamaa ambayo iliwafanya wasimamizi wa Unikolai kuunganisha serikali na kanisa kwa sababu walijua utajiri na mamlaka waliyopata. Kwa kuwa Wakati wa Efeso ulikuwa ni tuta tu kwa Wakati ule wa huzuni sana wa Pergamo ambao ulikuwa bado ni wa siku zijazo, Wakati huu wa Smirna ulikuwa ndio mvua, jua, na chakula kilichohakikisha uovu mbaya sana ambao ungeliimarisha kanisa katika ibada za sanamu ambazo ni uzinzi wa kiroho, ambamo kanisa

halingeweza kutoka humo kamwe. Mauti ilikuwa ikipenya katika mizizi yake hadi kwenye matawi na wale walioshiriki naye, walishiriki uchungu wa mauti. Wakati huu ulidumu kutoka 170 hadi 312 A.D.

**SALAMU**

Ufunuo 2:8,

> *"Haya ndiyo anenayo Yeye aliye wa Kwanza na wa Mwisho, Aliyekuwa amekufa, kisha akawa hai."*

*"Wa Kwanza na wa Mwisho Aliyekuwa amekufa kisha akawa hai."* Sasa haya si maneno ya mwanadamu. Mtu wa kawaida (kama angaliweza kunena kutoka kaburini) angesema, "Mimi ni wa kwanza na wa mwisho aliyekuwa anaishi na sasa amekufa." Jambo la kwanza linalompata mtu ni kwamba anazaliwa (anaishi) na jambo la mwisho linalompata ni kwamba yeye anakufa. Kwa hiyo huyu si mtu anayenena. Huu ni Uungu. Mwanadamu (Adamu) alichukua uhai na kuubadilisha ukawa mauti. Bali mtu huyu (Yesu) alichukua mauti na kuyageuza yakawa uzima. Adamu alichukua kutokuwa na hatia akakugeuza kuwa hatia. Huyu alichukua hatia akaigeuza kuwa haki. Adamu alichukua paradiso akaigeuza ikawa nyika tupu inayovuma; lakini Huyu anarudi kuigeuza dunia inayopepesuka na kuyumbayumba kwa maangamizi iwe Edeni nyingine. Adamu alichukua maisha ya ushirika na ya furaha pamoja na Mungu na kuyageuza kuwa jangwa la giza la kiroho lililosababisha dhambi zote, kuoza kwa uadilifu, maumivu, mateso, udanganyifu, na upotovu ambavyo hufanya vita katika nafsi za wanadamu. Lakini Huyu, kutoka kwenye mauti yote yenye huzuni na uzinzi uliowajaa wanadamu, akaleta maisha ya haki na uzuri, hivi kwamba kama vile dhambi wakati mmoja ilivyotawala hata mauti, vivyo hivyo watu wanaweza sasa kutawala katika haki kwa Mmoja, Kristo Yesu; na si vile hilo kosa lilivyokuwa, ingawa lilikuwa baya sana, lakini zaidi sana sasa kipawa Chake cha uzima wa milele kinatawala katika haki kwa njia ya Mtu mmoja.

Naye yuko hapa, akienda katikati ya wale ambao Yeye amewakomboa, yaani kanisa Lake. Na wale waliokombolewa walikuwa nini? Je! wengi hawakuwa kama Paulo, wauaji na waovu? Je! wengi hawakuwa kama yule mwizi aliyekuwa anakufa, wanyang'anyi na wauaji wa watu? Wote ni tuzo za neema Yake. Wote walifufuliwa kutoka kwa wafu. Wote wamefanywa HAI katika Kristo Yesu, Bwana.

Nashangaa kama mliiona salamu hiyo kwa wakati wa kwanza kisha mkaiangalia ile ya wakati huu. Hebu ziweke zote pamoja tu. "Haya ndiyo asemayo Yeye azishikaye hizo nyota saba katika mkono Wake wa kuume na Yeye aendaye katikati ya yale makanisa. Haya ndiyo asemayo wa Kwanza na wa Mwisho, Aliyekuwa amekufa kisha akawa hai." Huyu ni mtu yule yule. Naye anatujulisha ya kwamba kanisa ni Lake.

Kama vile mbegu ya tunda ilivyo katikati ya tunda, ndivyo alivyo Yeye, Uzao wa Kifalme, katikati ya kanisa. Kama vile mbegu peke yake ilivyo na uhai ndani yake, vivyo hivyo Yeye Ndiye mwanzilishi wa uzima kwa kanisa. Kutembea Kwake kunaonesha kulishughulikia Kwake bila kuchoka. Yeye ni Mchungaji Mkuu akiwalinda walio Wake. Hiyo ni haki Yake, kwa maana alilinunua kanisa hilo kwa damu Yake mwenyewe. Hiyo damu ni damu ya Mungu. Yule anayemiliki kanisa hilo ni Mungu, Mungu mwenyewe. Yeye Ndiye wa "Kwanza na wa Mwisho." Sifa hiyo inamaanisha umilele. Alikuwa amekufa na sasa yu hai. Yeye alilipa gharama ili awe na umiliki pekee wa hekalu la Mungu. Yeye analitawala. Yeye anaabudiwa ndani yake. Yeye anachukia ye yote anayechukua Uongozi Wake na mamlaka. Si ajabu sababu ya Yeye kujitambulisha Mwenywe kwa kila wakati kama Mungu ni kuwaonya na kuwafariji watu. Yeye huonya mzabibu wa uongo, na huufariji mzabibu wa kweli. Huyu Ndiye yule MUNGU MMOJA WA KWELI MWENYEZI. Msikieni mpate kuishi.

**HALI ZA WAKATI ULE**

Ufunuo 2:9,

> *"Nayajua matendo yako na dhiki yako, na umaskini wako, (lakini wewe u tajiri), najua na matukano ya hao wasemao ya kuwa ni Wayahudi, nao sio, bali ni sinagogi la Shetani."*

Ufunguo kwa wakati huu bila shaka kabisa ni dhiki. Kama kulikuweko na dhiki katika wakati wa kwanza, sasa kumetabiriwa kuongezeka kwa dhiki katika wakati wa pili wote. Hapana shaka ila haya maneno yafuatayo ya Paulo yalitumika kwa wengi wa Wakristo po pote walipokuwa duniani na katika kila wakati.

Waebrania 10:32-38,

> *"Lakini zikumbukeni siku za kwanza, ambazo, mlipokwisha kutiwa nuru, mlistahimili mashindano makubwa ya maumivu;*
>
> *Pindi mlipotwezwa kwa mashutumu na dhiki, na pindi mliposhirikiana na wale waliotendewa hayo, maana mliwaonea huruma wale waliokuwa katika vifungo,*
>
> *Maana mliwaonea huruma wale waliokuwa katika vifungo, tena mkakubali kwa furaha*

*kunyang'anywa mali zenu, mkijua nafsini mwenu kwamba mna mali iliyo njema zaidi, idumuyo mbinguni.*

*Basi msiutupe ujasiri wenu, kwa maana una thawabu kuu.*

*Maana mnahitaji saburi, ili kwamba mkiisha kuyafanya mapenzi ya Mungu mpate ile ahadi.*

*Kwa kuwa bado kitambo kidogo sana, na Yeye ajaye atakuja, wala hatakawia.*

*Sasa mwenye haki wangu ataishi kwa imani; Naye akisita-sita, roho yangu haina furaha naye."*

*Kule kuungana tu kwa watu wema na mwamini halisi huenda kukasababisha mauti kabisa badala ya wema wao.*

Sasa Bwana Mungu Mwenyezi asema, "NAJUA." Huyo hapo anatembea katikati ya watu Wake. Huyo hapo, Mchungaji Mkuu wa kundi. Lakini je! Yeye anazuia mateso? Je! Yeye husimamisha ile dhiki? La, Yeye hafanyi hivyo. Yeye anasema tu "NAJUA dhiki yako_si kwamba sijali mateso yenu hata kidogo." Jinsi hili lilivyo jiwe la kukwaza kwa watu wengi. Kama vile Israeli wanajiuliza kama Mungu kweli anawapenda. Mungu anawezaje kuwa mwenye haki na mwenye upendo kama Yeye anasimama karibu na kuwaona watu Wake wakiteseka?

Hivyo ndivyo walivyouliza katika Mal. 1:1-3,

*"Ufunuo wa Neno la Bwana kwa Israeli kwa mkono wa Malaki.*

*Nimewapenda ninyi, asema Bwana. Lakini ninyi mwasema, Umetupendaje? Je! Esau hakuwa ndugu yake Yakobo? asema Bwana; ila nimempenda Yakobo*

*Bali Esau nimemchukia na kuifanya milima yake kuwa ukiwa, na urithi wake nimewapa mbweha wa nyikani."*

Mnaona, hawakuweza kujua upendo wa Mungu. Walidhani ya kwamba upendo haumaanishi mateso. Walidhani ya kwamba upendo ulimaanisha mtoto mchanga anayelelewa na wazazi. Lakini Mungu alisema ya kwamba upendo Wake ulikuwa upendo wa "kuteuliwa." Thibitisho la upendo Wake ni KUTEULIWA_ya kwamba haidhuru nini kingetutukia, upendo Wake ulithibitishwa kwa kweli kwa ukweli kwamba wao walichaguliwa hadi wapate wokovu (kwa maana Mungu amekuchagua upate wokovu kwa njia ya utakaso wa Roho na kuiamini ile kweli). Yeye anaweza kukuacha uuawe kama vile alivyomwacha Paulo. Anaweza kukuweka katika mateso kama alivyomtendea Ayubu. Hiyo ni haki Yake. Yeye ni mwenyezi. Lakini yote ni kwa kusudi. Kama hangekuwa na kusudi fulani, basi Yeye angekuwa mwanzilishi wa mgogoro wala si wa amani. Kusudi Lake ni kwamba baada ya sisi kuteseka kwa muda kidogo tungefanywa wakamilifu, tuimarishwe, tutiwe nguvu na kupewa raha. Kama alivyosema Ayubu, "Yeye hututia nguvu." (Ayubu 23:6b) Mnaona Yeye, Mwenyewe, aliteseka. Alijifunza kutii kwa mateso hayo yaliyompata. Kwa kweli alikamilishwa kwa mateso hayo yaliyompata.

Waebrania 5:8-9,

*"Ingawa ni Mwana, alijifunza kutii kwa mateso hayo yaliyompata;*

*Naye alipokwisha kukamilishwa, akawa sababu ya wokovu wa milele kwa watu wote wanaomtii."*

Katika lugha dhahiri, utu wenyewe wa Yesu Kristo ulikamilishwa kwa mateso. Na kulingana na Paulo Yeye ameachia kanisa Lake sehemu ya mateso ili kwamba wao, pia, kwa imani yao katika Mungu huku wakiteseka kwa ajili Yake, wangefikia mahali pa ukamilifu. Kwa nini alitaka jambo hili?

Yakobo 1:2-,

*"Ndugu zangu, hesabuni ya kuwa ni furaha tupu, mkiangukia katika majaribu mbalimbali;*

*Mkifahamu ya kuwa kujaribiwa kwa imani yenu huleta saburi.*

*Saburi na iwe na kazi kamilifu, mpate kuwa wakamilifu na watimilifu bila kupungukiwa na neno."*

Kwa nini anasimama kando? Sababu yake ni katika Warumi 8:17-18,

*"Na kama tu watoto, basi, tu warithi; warithi wa Mungu, warithio pamoja na Kristo; naam, tukiteswa pamoja Naye ili tupate na kutukuzwa pamoja Naye.*

*Kwa maana nayahesabu mateso ya wakati huu wa sasa kuwa si kitu kama utukufu ule*

*utakaofunuliwa kwetu.*"

Tusipoteseka pamoja Naye hatuwezi kutawala pamoja Naye. Huna budi kuteseka upate kutawala. Sababu ya jambo hili ni kwamba tabia kamwe haiumbiki bila mateso. Tabia ni USHINDI, si karama. Mtu asiye na tabia hawezi kutawala kwa sababu mamlaka isiyo na tabia ni ya Kishetani. Lakini mamlaka iliyo na tabia inastahili kutawala. Na kwa kuwa Yeye anataka sisi tushiriki hata kiti Chake cha enzi kwa msingi ule ule ambapo Yeye alishinda na kuketi katika kiti cha enzi cha Baba Yake, basi hatuna budi kushinda tupate kuketi pamoja Naye. Na yale mateso madogo yasiyodumu tunayopitia sasa hayastahili yakilinganishwa na utukufu ulio mkuu sana utakaofunuliwa ndani yetu wakati atakapokuja. Loo! ni hazina za jinsi gani zilizowekewa akiba wale walio tayari kuingia katika ufalme Wake kupitia kwenye dhiki.

*"Msione kuwa ni ajabu ule msiba ulio kati yenu, unaowapata kama moto ili kuwajaribu."*

Hivyo ndivyo Petro alivyosema. Je! ni ajabu kwamba Mungu anatutaka tupate tabia kama ya Kristo inayokuja katika mateso? La bwana. Nasi sote tuna majaribu. Sote tunajaribiwa na kurudiwa kama wana. Hakuna hata mmoja asiyepitia katika hayo. Kanisa ambalo haliteseki, wala halijaribiwi, limekosa_si la Mungu.

Ebr. 12:6,

> *"Maana yeye ambaye Bwana ampenda, humrudi, Naye humpiga kila mwana amkubaliye. Basi kama mkiwa hamna kurudiwa, ambako ni fungu la wote, ndipo mmekuwa wana wa haramu ninyi, wala si wana wa halali."*

Sasa hali hii maalum katika Smirna haina budi kutumiwa kwa kila wakati. Hakuna wakati usio na hali hiyo. Hakuna mwamini wa kweli asiye na hali hiyo. Hili ni la Mungu. Haya ndiyo mapenzi ya Mungu. Linahitajika. Tunamhitaji Bwana atufundishe ile kweli ya kwamba hatuna budi kuteseka na kuwa kama Kristo katika kufanya jambo hilo. *"Upendo huvumilia na hufadhili."*

Mathayo 5:11-12,

> *"Heri ninyi watu watakapowashutumu na kuwaudhi na kuwanenea kila neno baya kwa uongo, kwa ajili Yangu.*
>
> *Furahini, na kushangilia; kwa kuwa thawabu yenu ni kubwa mbinguni; kwa maana ndivyo walivyowaudhi manabii waliokuwa kabla yenu.*"

Anga zenye mawingu na dhoruba za maisha si ishara za kukataliwa na Mungu. Wala anga nyeupe na maji matulivu si ishara za upendo wa Mungu na kibali Chake. Kibali Chake kwa ye yote wetu kiko katika YULE MPENDWA. Upendo Wake ni wa kuchagua ambao alitupenda nao kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Je! Yeye anatupenda? Naam ndiyo. Lakini tutajuaje? Tutajua kwa sababu Yeye ALISEMA HIVYO, na akadhihirisha ya kwamba alitupenda kwa kuwa alituleta Kwake na akatupa Roho Wake, akituweka kama wana. Nami nitathibitishaje upendo wangu Kwake? Kwa kuamini yale aliyosema, na kwa kuenenda kwa furaha katikati ya majaribio ambayo Yeye katika hekima Yake anayaruhusu yatimie.

*"Najua umasikini wako (bali wewe ni tajiri)."*

Hilo hapo tena. Mtazame akitembea hapa na pale katikati ya Kanisa Lake. Kama vile baba Yeye anaiangalia familia Yake. Yeye ni Kichwa cha nyumba Yake. Yeye ndiye mtoa mahitaji. Yeye ndiye mlinzi. Hata hivyo Yeye anautazama umaskini wao. Loo! jinsi mwamini asiyefunzwa anavyojikwaa kwenye jambo hili. Mungu anawezaje kuvumilia kuwaangalia walio Wake wakati wa upungufu na asizuie jambo hilo lote_ajitolee na kuwafurahisha na kila kitu?

Hapa ndipo ambapo huna budi kuamini tena katika upendo, na wema na hekima ya Mungu. Hili, pia, linahitajika. Kumbukeni, Yeye alionya, "Msisumbukie ya kesho, mle nini au mnywe nini. Baba yenu anajua mambo mnayohitaji. Yeye anayeyavika maua na kuwalisha shomoro atawafanyia mengi zaidi. Vitu hivi vya kimwili si mahitaji yaliyo muhimu ya maisha yenu, kwa maana uzima wa mtu haumo katika wingi wa vitu vyake alivyo navyo. Bali heri utafuteni kwanza ufalme wa Mungu na haki Yake na vitu vyote vya kimwili mtaongezewa."

Watu wa Mungu si watu wa kupenda mali. Wao wanampenda Kristo. Wao hawatafuti hazina zilizo za dunia; wanazitafuta zilizo juu. Ni kweli kabisa, Wakristo walio wengi SI matajiri. Bali wao wako upande wa maskini. Ilikuwa hivyo katika siku za Yesu. Ilikuwa ni kweli katika siku za Paulo na inapaswa kuwa kweli leo. Loo! si kweli kabisa leo kwa kuwa Wakati wa Laodikia ni wakati wenye utajiri sana ambapo mara nyingi kipimo cha kuwa wa kiroho ni wingi wa mali ya dunia. Jamani, jinsi kanisa lilivyo tajiri katika mali. Lakini ni maskini iliyoje katika Roho. "Heri ninyi mlio maskini, kwa maana ufalme wa Mungu ni wenu. Ufalme wa Mungu SI kula na kunywa." Si wa kimwili. Umo NDANI yetu. Tajiri ni aliye tajiri katika Mungu, si katika vitu vya ulimwengu.

"Loo!" Roho anapaza sauti, "Ninaona umaskini wenu. Ninaona mahitaji yenu. Hamna vitu vingi, iwapo

mna cho chote kile, cha kujisifia. Yale mliyokuwa nayo mmenyang'anywa. Kwa furaha mlitoa mali zenu makazibadilisha na zile za milele. Mnachekwa. Mnadhihakiwa. Hamna mali mliyojiwekea akiba mnayoweza kutegemea. Lakini ninyi ni tajiri mbali na hayo yote. Usalama wenu umo katika Yeye aliye ngao yenu na thawabu kuu sana. Ufalme wenu haujaja bado. Lakini utakuja. Na utakuwa ni wa milele. Naam, ninayajali majaribu yenu na majonzi yenu. Ninajua jinsi ilivyo vigumu kuishi. Lakini nitakumbuka mambo haya yote nitakaporudi kuwachukua walio Wangu, ndipo nitawajazi."

Sasa hii si kuwapinga matajiri kwa sababu Mungu anaweza kumwokoa tajiri. Baadhi ya watoto wa Mungu ni matajiri. Lakini pesa zinaweza kuwa mtego sana, si kwa wale walio nazo tu bali kwa wale wasio nazo. Huko nyuma kabisa katika wakati wa kwanza, Yakobo aliwakemea wale waliokuwa wakiwategemea matajiri, "Imani ya Bwana wetu Yesu Kristo msiwe nayo kwa kupendelea watu." Maskini kule walikuwa wakijaribu kujipendekeza kwa matajiri kusudi wapate msaada, badala ya kumtegemea Mungu. "Usifanye hivyo," asema Yakobo. "Usifanye hivyo. Pesa si kila kitu. Pesa si jibu." Wala leo si jibu. Tuna mali nyingi zaidi ya tulivyopata kuwa nayo na hata hivyo ni machache yanayotimizwa Kiroho. Mungu hafanyi kazi kwa pesa. Yeye hutenda kazi kwa Roho Wake. Na kutenda huko kwa Roho huja tu kwa maisha yaliyowekwa wakfu kwa Neno.

**SINAGOGI LA SHETANI**

Ufunuo 2:9b.

> *"Najua na matukano ya hao wasemao ya kuwa ni Wayahudi, nao sio, bali ni sinagogi la Shetani."*

Hii hapa aya ambayo itahitaji kufikiriwa sana, si kwa sababu tu sababu ni ya kipekee sana katika maneno yake, lakini pia kwa kweli imerudiwa katika wakati ambao ni wa zaidi ya miaka elfu moja baadaye.

Ufunuo 2:9

> *"Nayajua na matendo yako na dhiki yako, na umaskini wako, (lakini wewe u tajiri), najua na matukano ya hao wasemao ya kuwa ni Wayahudi, nao sio, bali ni sinagogi la Shetani."*

Kwanza, neno, *Wayahudi*, halielezei dini ya Wayahudi. Linahusu tu watu wa Yuda na lina maana ile ile halisi kama ningalisema mimi nimezaliwa Muairishi. Watu hawa walikuwa wakisema ya kwamba walikuwa Wayahudi hasa, Wayahudi halisi kwa kuzaliwa. Walikuwa waongo. Hawakuwa Wayahudi kwa kuzaliwa na hawakuwa Wayahudi kwa dini.

Kama jambo hili lote ni kweli, wao walikuwa ni akina nani? Walikuwa ni watu waliodanganywa ambao tayari walikuwa sehemu ya kanisa. Walikuwa ni wa mzabibu wa uongo.

Hawakuwa wa kanisa la kweli, lakini wa kanisa la uongo kwa sababu Mungu alisema "walikuwa wa sinagogi la Shetani." Sasa neno litumikalo kwa sinagogi si neno lile lile tunalotumia kwa kanisa. Katika Biblia, kanisa maana yake ni, "walioitwa watoke", ama "walioalikwa". Mwandishi wa Zaburi alisema kuhusu watu hawa walioteuliwa,

> *"Heri mtu yule UMCHAGUAYE, na KUMFANYA akukaribie Wewe, apate kukaa nyuani Mwako."*

Zaburi 65:4.

Lakini maana ya sinagogi ni "kusanyiko ama mkutano." Huu unaweza kuwa mzuri ama mbaya, lakini kuhusiana na jambo hili ni mbaya, kwa maana hawa ni wale ambao kukusanyika kwao si kwa Mungu bali ni kwa wao wenyewe. Isaya alisema juu yao,

> *"Tazama, yamkini watakusanyana; lakini SI KWA SHAURI LANGU: Watu wo wote watakaokusanyana juu yako wataanguka kwa ajili yako."* Isa. 54:15.

Na kwa sababu hawa kweli walikuwa dhidi ya ule mzabibu wa kweli, Mungu siku moja atawashughulikia katika maangamizi.

Sasa kwa nini tuna watu waliochanganyikana katika mfumo wa kanisa na kujiita Wayahudi? Sababu ni hii: Kwa kuwa walikuwa waongo wangeweza kudai lolote walilotaka. Wangeweza kusema walilotaka kana kwamba ilikuwa ni kweli na halafu walishikilie. Na kwa jinsi hii wangeweza kudanganya wakiwa na wazo lenye nguvu sana moyoni mwao. Je! haikuwa hivyo kwamba kanisa la hapo mwanzoni lilikuwa lote ama karibu lote ni la Wayahudi, likiwafanya wao kuwa washiriki asili wa mwili Wake? Wale mitume kumi na wawili walikuwa ni Wayahudi, na mitume wa baadaye walikuwa ama Wayahudi ama waongofu. Kwa hiyo watu kuapa ya kwamba wao etini Wayahudi kungewapa utawala na dai la kuwa waanzilishi asilia. Sema uongo. Ushikilie. Kamwe usijali ukweli wala historia. Usema tu na uendelee kuusema kwa watu, na hivi karibuni watu wataupokea.

Sasa umekamata kitu fulani hapo? Hiyo si ni roho yule yule aliyeko kanisani leo? Je! hakuna kundi linalodai ya kwamba wao ndio kanisa la asili na la kweli na kwamba wokovu unapatikana tu katika hilo? Je! wao hawadai ya kwamba wana funguo za ufalme ambazo walizipokea kutoka kwa Petro? Je! wao hawadai ya kwamba Petro alikuwa ndiye papa wao wa kwanza, na ya kwamba yeye aliishi Rumi wakati ambapo HAKUNA KATAKATA KWELI YA HISTORIA YA JAMBO HILO? Na hata wafuasi wake wasomi hasa na wenye ujuzi sana wanaamini uongo wake. Sinagogi la Shetani! Na kama Shetani ndiye baba wa kanisa hilo, na yeye ni baba wa uongo, basi silo jambo la kushangaza ya kwamba hao walio kwenye sinagogi lake ni waongo pia.

Fikiria wazo la kukufuru. Hawa walio wa sinagogi la Shetani hawakuwa wakimkufuru Mungu katika jambo hili (ingawa jambo hilo ni wazi kabisa) lakini walikuwa wakilitukana kanisa la kweli. Hakika. Kama vile Kaini alivyomtesa na kumwua Habili kwa sababu yeye (Kaini) alikuwa wa yule mwovu, na kama vile wafuasi waliokufa wa Dini ya Kiyahudi (Yesu alisema walikuwa ni wa baba yao, ibilisi) walivyokuwa wakijaribu kuwaangamiza Wakristo katika miaka michache ya kwanza ya wakati wa kwanza, sasa kundi lili hili (mzabibu wa uongo) linajaribu hata kwa nguvu zaidi kumwangamiza mwamini wa kweli katika wakati wa pili. Roho hiyo ya mpinga-Kristo inakua.

Kundi ambalo lilijipenyeza pole pole kanisani kwa MATENDO yake (Unikolai) haliogopi tena kufunuliwa lakini limeunda madhehebu waziwazi katika kundi la kukusanyika kwake lenyewe na linalipinga kanisa la kweli katika uadui wa waziwazi.

Sasa wakati ninaposema ya kwamba hili lilikuwa kanisa la mpinga-Kristo lililokuwa madhehebu ninawaambia kweli ya historia iliyothibitishwa. Kanisa la kwanza lililoanzishwa Rumi (tutafuatilia historia yake katika Wakati wa Pergamo) lilikuwa tayari limebadilisha kweli ya Mungu kuwa uongo kwa kuingiza dini ya kipagani iliyokuwa na majina na maana ya Kikristo. Kufikia wakati wa pili lilikuwa la kipagani sana (ingawa lilikuwa linadai ati ndilo kanisa la kweli) hata Polikapu alipokuja yapata maili 1500 akiwa mzee sana kuwasihi warudi. Hawangekubali. Wao walikuwa na utaratibu wa ukuhani uliyo imara na madhehebu imara, na kuondoka kabisa kutoka kwenye Neno. Hili basi, ndilo sinagogi la Shetani, lililojaa makufuru, ambamo mlikuwemo tayari na mbegu za fundisho la Unikolai, na ambalo siku si nyingi lingekuwa kiti chenyewe ama nguvu za dini ya Kishetani. Na jambo hili ni kweli kabisa kwa kuwa Ufu. 2:9b HAUSEMI hawa watu ni WA sinagogi la Shetani lakini linasema wao NI SINAGOGI LA SHETANI.

Roho hii ya mpinga-Kristo si mpya. Hili si jambo lililokuja tu katika nyakati za kanisa. Limekuwapo hapa wakati wote. Ili kupata ufahamu dhahiri wa jinsi inavyotenda kazi, jinsi inavyompinga Mungu na kuchukua mamlaka ya juu ya kanisa, angalia kwenye Agano la Kale na uione kule. Hebu tuangalie roho hii kama ilivyodhihirishwa katika Israeli walipotoka Misri kuwa kanisa nyikani.

Kama tu vile kanisa la mwanzo lilivyoanza chini ya huduma safi ya Roho Mtakatifu likiwa na ishara na maajabu na madhihirisho kama vile unabii, lugha, na tafsiri, hekima, maarifa na uponyaji, vivyo hivyo katika siku za Israeli wakati walipoondoka Misri, wao walikuwa chini ya uongozi wa Roho wa Mungu akijidhihirisha katika karama. Mungu alikuwa ndiye kiongozi wa watu. Kwa kweli Yeye alikuwa Mfalme wao. Yeye alikuwa Baba-Mfalme. Aliishughulikia Israeli kama vile mtu anavyoiangalia familia yake. Yeye aliwalisha, akapigana vita vyao, akawaondolea shida zao na kutatua shida zao. Yeye alijishughulisha sana nao. Wao walikuwa ndio taifa la pekee ambalo kwake Yeye ndiye aliyekuwa Mungu wao kwa kweli. Lakini siku moja wakaanza kutupa macho huko na huko, ndipo wakawaona Wafilisti na mataifa mengine wakiwa na wafalme juu yao. Likawavutia nao wakaamua ya kwamba wanapaswa kuufanya uongozi wao kuwa wa kibinadamu, kwa hiyo wakataka mfalme. Sasa Mungu Mwenyewe alikuwa yuaenda kuufanya uongozi wao kuwa wa kibinadamu, katika Utu wa Bwana Yesu Kristo, lakini wao wakamtangulia. Shetani alijua mpango wa Mungu kwa hiyo akaliweka katika mioyo ya watu wamtangulie Mungu (Neno).

Wakati walipomwendea Samweli na kuomba wapewe mfalme, Samweli alifadhaika sana hata roho yake karibu izimie. Mungu alikuwa anawaongoza watu Wake kupitia kwa nabii huyu aliyewekwa wakfu, aliyethibitishwa kwa Maandiko naye akaona kwamba alikuwa amekataliwa. Aliwakusanya watu na kuwasihi wasimwache Mungu ambaye alikuwa amewabeba kama watoto, na akawafanikisha na kuwabariki. Lakini wao wakakaidi. Wakamwambia Samweli. "Hujawahi kukosea katika uongozi wako. Hujawahi kuwa mdanganyifu katika shughuli zako za fedha. Umejaribu uwezavyo kutuweka sawa na Neno la Bwana. Tunaifurahia miujiza, hekima, chakula na ulinzi wa Mungu. Tunauamini. Tunaupenda. Na isitoshe hatutaki kuukosa. Ni kwamba tu tanataka mfalme wa kutuongoza vitani. Sasa bila shaka tunapotoka kwenda vitani yangali ni makusudio yetu kuacha makuhani watutangulie huku Yuda wakifuata, nasi tutapiga matarubeta na kupiga makelele na kuimba. Hatutarajii kuacha yo yote ya mambo hayo. LAKINI TUNATAKA MFALME AMBAYE NI MMOJA WETU APATE KUTUONGOZA."

Ndipo Mungu akamwambia Samweli. "Mnaona, wao hawakukukataa wewe, lakini wamenikataa MIMI nisiwatawale."

Jinsi hilo lilivyokuwa la kusikitisha. Hawakutambua ya kwamba wakati walipokuwa wakimwomba Mungu awaache wawe kama wengine wa ulimwengu walikuwa wakimkataa, kwa sababu Mungu alikuwa

ameamuru kwamba watu Wake waenende tofauti na ulimwengu. Wao si wa ulimwengu wala hawaonekani kama ulimwengu wala hawatendi kama ulimwengu. Wamesulibiwa kwa ulimwengu na ulimwengu umesulibiwa kwao.

II Wakorintho 6:17-18,

> *"Kwa hiyo tokeni kati yao, mkatengwe nao, asema Bwana, msiguse kitu kilicho kichafu; nami nitawakaribisha,*
>
> *Nitakuwa Baba kwenu, nanyi mtakuwa Kwangu wanangu wa kiume na wa kike, asema Bwana Mwenyezi."*

Mnaona tofauti moja kati ya Israeli na mataifa mengine ilikuwa ni Mungu. Mweke Mungu upande mmoja na Israeli walikuwa kama taifa lingine lo lote. Wakati Samsoni alipokata nywele zake alikuwa kama mtu mwingine yeyote. Weka uongozi wa Roho Mtakatifu kando na kanisa si KITU CHO CHOTE ILA ULIMWENGU ULIOBANDIKWA JINA LA MUNGU. Ulimwengu na kanisa vyote ni fungu moja, kama tu vile Yakobo na Esau walivyokuwa wa wazazi wale wale, lakini Roho wa Mungu ndiye anayeleta tofauti.

Haijalishi kama unajiita Mkristo. Mtu yeyote anaweza kufanya hivyo. Jambo la msingi ni kama una Roho wa Mungu ndani yako ama la, kwa kuwa bila Roho huyo umekataliwa; wewe si wake. Amina.

Si muda mrefu uliopita nilimwuliza mama mmoja kama alikuwa Mkristo. Akaniambia, "Sina budi kukujulisha, bwana, ya kwamba mimi huwasha mshumaa kila usiku." Hivi jambo hilo lina uhusiano gani na hilo? Mimi ni Mmethodisti, mimi ni Mbaptisti, mimi ni Mpentekoste. Hilo halina uhusiano wowote nalo. Ni Roho Mtakatifu ama utaangamia.

Vema, wakianzia kule nyuma kabisa katika kanisa la kwanza watu kufikiria na kuhoji jinsi ya kuboresha mahusiano na Mungu vizuri zaidi. Matendo ya Wanikolai yalianza kujionesha. Halafu kundi fulani likaundwa. Wakaondoka kwenye utaratibu wa Neno. Yote yanayohitajika ni kubadilishwa kwa Neno moja tu ndipo chachu hiyo ndogo inachachua donge lote. Yeye anayejikwaa katika neno moja la sheria amekosa juu ya yote. Hawa alibadilisha tu neno moja. Hilo litatosha.

Na wakati kundi hilo la Kishetani lilipoundwa, lilianza kuwachukia na kuwapiga vita waamini wa kweli, likisisitiza ya kwamba wao (hao wageni) walikuwa ndio kanisa la Mungu.

Angalia jinsi madhehebu yanavyozaa chuki. Huharibu ushirika. Husababisha uchungu. Hiyo ndiyo maana ya manemane. Huu ndio ulikuwa umejaa Smirna. Uchungu. Shina la uchungu huwatia wengi unajisi. Kwa hiyo unajisi zaidi na zaidi ulikuwa ukiingia. Kila wakati wa kanisa ungehisi makovu yake.

Kanisa la Smirna lilikuwa limeenda mbali na lile la mwanzo. Lilikuwa limekuwa chotara. Lilikuwa limechanganya mbegu kama vile Hawa alivyofanya. Unajua kwamba chotara ni matokeo ya kuchanganyika jamii ya vitu viwili vinavyofanana. Matokeo yake si kiumbe kilicho safi tena kama kile cha asili. Ni chotara. Vema, wakati Hawa alipomruhusu yule mnyama wachanganye mbegu zao alizaa kiumbe aliyeitwa Kaini ambaye hakuwa mwanadamu halisi. Yeye alikuwa wa YULE MWOVU. Angalia jinsi alivyokuwa tofauti na Habili. Angalia jinsi alivyokuwa tofauti na Sethi. Yeye alimchukia Mungu wala hangetii Neno na alimtesa na kumwua mwenye haki. Alijiweka juu ya Neno la Mungu.

Kanisa, pia, limeondoka kutoka kile lilichokuwa hapo awali. Yeye ni chotara. Hiyo ni kusema, kanisa la kawaida ni chotara. Watu husema, "Mimi ni Mbatisti." Haikuwa hivyo hapo mwanzo. "Mimi ni Mmethodisti." Haikuwa hivyo hapo mwanzo. Badala ya Neno la moja kwa moja la Mungu, badala ya watu waliojazwa Roho katika kanisa ambao walikuwa wameongozwa na ufunuo uliotolewa na Roho, sasa kuna kanuni za imani, na sheria, na mabahatisho ya kielimu ya watu wenye elimu. Kujifunza kumechukua mahali pa ufunuo. Hoja zimechukua nafasi ya imani. Taratibu zimechukua mahali pa sifa zinazobubujika zenyewe katika Roho Mtakatifu. Haikuwa hivyo tangu mwanzo. Jamii yote imebadilika. Limekuwa kanisa chotara.

Sasa basi, kanisa linapokuwa chotara, je! litazaa Wakristo halisi? Haliwezi. Uhai ama mbegu inayowazaa Wakristo haimo ndani yao. Kila mbegu huzaa kwa jinsi yake. Wabaptisti huzaa Wabaptisti wengi zaidi na wanatenda kama Wabaptisti. Wamethodisti huzaa Wamethodisti nao wanatenda kama Wamethodisti. Hakuna hata mmoja anayejulikana kwa nguvu za Mungu wala hawezi kuwa kwa maana hayupo. Yanajulikana kwa desturi zao za ibada ya Mungu na kanuni zao za imani na mafundisho yao ya sharti.

Nena kuhusu chotara. Je! Mnajua chotara maarufu sana ulimwenguni? Amekuwa pamoja nasi kwa miaka mingi. Ni nyumbu. Ni kuchanganya mbegu kati ya punda na farasi. Yeye ni mnyama wa kuchekesha. Hawezi kuzaa nyumbu mwingine. Yeye hana uhai unaoweza kufanya hivyo. Hata hivyo nena kuhusu kazi. Anaweza kufanya kazi zaidi ya farasi ama punda. Lakini angalia asili yake. Yeye ni mkaidi na kamwe huwezi kumwamini. Yeye ni picha kamilifu ya dini chotara. Mchanganyiko baina ya kweli na giza, kwa maana farasi ni mfano wa mwamini wa kweli na punda ni picha ya yule mwovu. Wachanganye pamoja nawe unapata dini iliyo tasa, ya kawaida. Haina mbegu ya uzima. Imekufa. Inaweza kuzungumza

juu ya kweli lakini haiwezi kuidhihirisha. Haina Mungu ndani yake, hata hivyo inakusanyika pamoja na kuzungumza juu ya Mungu, na ikiwa wakati huo wote inakana zile nguvu kwa taratibu zao. Watalikana Neno katika Jina la Bwana. Na kamwe hakuna tumaini lolote kwao. Je! Mnatambua ya kwamba hakuna dini ya kimadhehebu iliyopata kuwa na uamsho? Kamwe! Mara walipounda madhehebu walikufa. Hawawezi kamwe kurudi. La bwana. Ninaweza kuwaonyesha jambo hilo kwa mfano.

Katika Kutoka 13:13,

> *"Kila mzaliwa wa kwanza wa punda utamkomboa kwa mwana-kondoo; na kwamba hutaki kumkomboa, utamvunja shingo; na kila mzaliwa wa kwanza wa binadamu katika wanao utamkomboa."*

Mnaona, punda anaweza kukombolewa. Kila maskini mwenye dhambi anaweza kukombolewa kwa damu ya sadaka ya Yesu Kristo, ama kwa kumkataa Kristo akataliwe mwenyewe. Lakini humkomboi nyumbu. Hakuna ukombozi kwa ajili yake. Hakuna damu kwa ajili yake. Haiwezekani kuwepo kwa sababu nyumbu hukimbilia kanisani ambapo punda anakimbilia kwenye ile damu. Nyumbu hana "mbegu" ndani yake ambayo inaweza kuhuishwa, lakini punda ana mbegu.

Mbona, majuma machache yaliyopita nilisoma maoni ya mhariri. Naam, yalikuwa ni maoni ya mhariri yaliyoandikwa na mfanyi biashara ambaye hajaokoka; si na Mkristo. Yeye alisema ya kwamba alishangazwa na makanisa. Asingeweza kuyaelewa. Yalikuwa na seminari zilizojaa maprofesa waliofundisha Neno la Mungu kusudi wapate kuliangamiza. Sasa basi mtu huyu asingeweza kutambua hilo. Alishangazwa sana nalo. Alisema ya kwamba aliweza kumwelewa kafiri ama mkomunisti, ama mtu mwenye mawazo huru ama mtu mwingine akifanya jambo hilo. Lakini wakati kanisa lenyewe linapoharibu Neno la Mungu ilikuwa ni sawa na mauaji ya kukusudia. HIYO HAPO DINI YAKO YA KISASA. AMKENI ENYI WAMAREKANI KABLA HAMJACHELEWA SANA.

Wakati kanisa linapoondoka kwenye Neno litaamini chochote. Ni kama Hawa. Wakati Kaini alipozaliwa Hawa alisema, "Nimepata mtoto mwanamume kwa Bwana." Sasa hivi mnatambua ya kwamba kweli yeye alimaanisha hivyo? Yeye alidhani alipata mtoto mwanamume kutoka kwa Bwana. Mnaona, mara alipodanganywa kwa kulichukua Neno la Shetani badala ya Neno la Mungu yeye basi alifikiri ya kwamba cho chote alichosema kilikuwa ni kweli. Kama alisema kwamba alipata mtoto mwanamume kutoka kwa Mungu, basi alimpata mtoto mwanamume kutoka kwa Mungu. Lakini Mungu ameweka sheria katika ulimwengu Wake. Mbegu njema inaweza tu kuzaa tunda zuri na mbegu mbaya inaweza tu kuzaa tunda baya. Sasa kila mbegu, ingawa ni tofauti, itatumia ardhi ile ile, chakula, unyevu, na jua, lakini itazaa kwa jinsi yake. Angalia historia ya ukoo wa Kaini. Angalia historia ya ukoo wa Sethi. Tofauti moja tu kati yao—ile mbegu ya asili. Hakuna kitu kingine.

Kama ukichunguza tamshi hili la Hawa kwa makini sana utaona ya kwamba yeye alipata ufahamu zaidi kuliko watu wengi wanavyotambua. Yeye hakusema mwanawe ni wa Shetani kwa maana jambo hilo lingemfanya kuwa sawa na Mungu. Mungu tu ndiye angeweza kuumba yai katika tumbo la uzazi la Mariamu. Shetani asingeweza kufanya jambo hilo. Hawa alijua jambo hilo. Shetani anaweza tu kupotosha. Kwa hiyo alimdanganya kwa mbegu mbaya. Ilikuwa ni uzao wa nyoka uliomzaa Kaini. Ilikuwa ni uzao wa Adamu uliomzaa Habili na Sethi. Mbegu hizo zilipitia kwenye hatua zile zile, lakini hao watoto walikuwa tofauti kwa maana walitokana na mbegu tofauti.

Aliamini ya kwamba Kaini alitoka kwa Mungu. Alikubali uongo wa ibilisi kama kweli ya Mungu. Hilo ndilo hasa tulilo nalo sasa. Makanisa yamejiweka kama chemchemi za kweli lakini kweli haimo ndani yao; hata hivyo watoto wao waliowazaa wanaapa kwa wao na hata wataua kusudi wadumishe kosa lao.

Kama unafikiri ya kwamba hilo ni kutia chumvi, soma II Timotheo sura ya 3 yote na aya za kwanza tano za sura ya nne.

II Timotheo 4:1-5

> *"Nakuagiza mbele za Mungu, na mbele za Bwana Yesu Kristo, atakayewahukumu walio hai na waliokufa; kwa kufunuliwa Kwake na kwa ufalme Wake;*
>
> *Lihubiri Neno, uwe tayari, wakati ukufaao na wakati usiokufaa, karipia, kemea, na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho.*
>
> *Maana utakuja wakati watakapoyakataa mafundisho yenye uzima; ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajipatia waalimu makundi makundi, kwa kuwa wana masikio ya utafiti;*
>
> *Nao watajiepusha wasisikie yaliyo kweli, na kuzigeukia hadithi za uongo.*
>
> *Bali wewe, uwe na kiasi katika mambo yote, vumilia mabaya, fanya kazi ya mhubiri wa Injili, timiliza huduma yako."*

Wakati kanisa lilipojiachilia liondoke kutoka kwenye lile la mwanzoni, kama Adamu na Hawa, mauti

iliingia.

Hakuna nguvu ndani yake. Limekuwa dubwana. Mara kanisa lilipoelekea kwenye mambo ya desturi na kawaida za dini, na kwenye ukuhani kwa kuwaingiza wahudumu katika kundi lililoamua uongozi mbali na Roho Mtakatifu na Neno Lake, wakati uo huo mauti iliingia nalo likaanza kuugua, na lilipokuwa gonjwa lilibadilika likawa kundi la watu wasio na nguvu ambao silaha yao pekee ni mabishano. Halikuweza kudhihirisha kitu cho chote katika Roho, kwa maana matumaini yake yalijengwa juu ya utaratibu wala si katika imani katika Neno Lake. Walipanda utaratibu kwa hiyo wakavuna utaratibu. Walipanda upotovu kwa hiyo wakavuna watoto waliopotoka.

Ukicheza na Mungu utavuna kile hasa ulichopanda. Mwanadamu anapaswa kujifunza hayo kutokana na maumbile. Yeye ameyaharibu maumbile. Ameingiza mawazo yake mwenyewe katika maumbile na kugeuza taratibu za molekiu, nk., na sasa yeye anavuna kimbunga. Hebu angalia tu jinsi walivyowazalisha kuku. Wamewazalisha kitaalam mno hivi kwamba kuku ni mashine ya kutaga inayojiua yenyewe kwa kutaga. Hafai kwa chakula na ni laini na hana ladha. Wao wanadunga vitu katika nyama tunayokula na kwa sababu ya jambo hilo mwili wa mwanadamu unabadilika hivi kwamba wanawake wanazidi kuwa na viuno vyembamba na mabega mapana na wanaume wanakuwa kinyume chake tu. Sasa kama ukichezea maumbile na upate kioja na mlipuko, itakuwaje kama ukigeuza kweli iwe uongo? Jibu ni, utazaa utaratibu wa dini ya upinga-Kristo, usio na Mungu ambao umepotoshwa sana hata hautafanana ama kuzaa kitu kama kile cha asili. Jibu pekee alilo nalo Mungu kwa hali kama hiyo ni lile ziwa la moto.

Wakati ule wa Smirna unaosikitisha ulikuwa unakufa. Wakati ulipokufa, haukurudi tena. Hakuna wakati wa knisa uliowahi kurudi tena. Hakuna ufufuo uliowahi kurudi kamwe. Hauwezi kuwa na uhai wa Mungu ndani yake kwa kuzaliwa kimwili. Kunatakiwa kuzaliwa mara ya pili kutoka juu. Wakati huu wa mwisho ulianza kwa mioto ya ufufuo wa Kipentekoste nao wakarudi kuunda madhehebu moja kwa moja. Badala ya kulichukua Neno wao walichukua mawazo yao wenyewe na kufanya yale yaliyofanywa na kila wakati_wakaweka kitabu kidogo cha mafundisho kiwe badala ya Neno. Hebu jaribu kuondoka kwenye kitabu hicho uone yatakayokupata. Utafukuzwa, ndugu. Nao watakutesa na kumlaumu Mungu kwa jambo hilo. Na jinsi wanavyoyapenda madhehebu yao. Si ajabu. Wao ni Wapentekoste wa kizazi cha pili na kwa kuwa Mungu hana wajukuu wao ni watoto tu wa baba zao, wanaojulikana kwa kanuni zao za imani na utaratibu wao wa ibada. Wanaweza kuzungumza juu ya jinsi mambo yalivyokuwa, lakini hawawezi kuyadhihirisha. Wakati fulani walikuwa na umeme lakini karibu yote yaliyosalia ni ngurumo.

Lakini hebu wakwambie juu ya utukufu wa shirika lao. Watasema, "Naam, bwana, nataka ujue ya kwamba shirika hili halikuanzishwa na mwanadamu. Lilizuka lenyewe tu. Roho alishuka kote ulimwenguni. Naam bwana, tulipata kile walichokuwa nacho Pentekoste. Hili halikuwa la wanadamu bali la Mungu." BASI MBONA WAO HAWAKULIDUMISHA JINSI HIYO? KAMA MUNGU ALILIANZISHA MBONA MUNGU ASIWEZE KULIDUMISHA NA KULIMALIZIA? Kama Mungu hakuandika kitabu kidogo cha kanuni za imani na utaratibu na mafundisho ya sharti kulianzisha, basi wao walikuwa na haki gani ya kufanya jambo hilo?

Mungu alimwaga Roho Wake juu ya Wabatisti, Wamethodisti, Wanazarayo, Wasabato, Wapresbiteri, Wandugu, Kanisa la Mungu (mengi yanavyojiita) nk. Ndugu hawa wote walikuzwa kwa mafundisho tofauti, sheria, vitabu vya mafundisho ya kanisa nk. Mungu aliyaondoa akayaweka upande mmoja; Yeye aliangamiza nadharia zao za vipindi vya wakati na akarudisha karama za Roho, akithibitisha ya kwamba ni yeye yule jana leo na hata milele. Lakini je! hao Wapentekoste walijuta kuhusu madhehebu? La bwana. Waliunda madhehebu tena na wameandika vitabu vyao wenyewe, sheria na vitabu vya kanisa, kitabu cha ushirika nk. wakiwa na wazo moja akilini mwao, ambalo ni kuthibitisha ya kwamba sasa wao wana majibu yote, wanajua majibu yote, na kwa hiyo wao ni watu bora wa Mungu waliosoma wanaojua njia na wanaweza kuwaonyesha njia wengine kama viongozi waliochaguliwa na Mungu. Bali hawana kitu. Wao ni chotara tu kama makundi yale yale walimotoka. Kama wao wanataka kuwa katika bibi-arusi itawabidi watoke kama vile hasa walivyofanya babu zao.

Wao ni kama wengine wote. Uamsho umekwisha. Wanajaribu kuishi jina fulani nao wamekufa. Walichukua madhehebu, wakati huo huo wakizungumzia kuhusu Roho wa Mungu. Wanazungumza juu ya thibitisho la Roho Mtakatifu. Lakini wanasahau ya kwamba ibilisi anaweza kunena kwa lugha, pia. Mchafuko mtupu wa Babeli uko katikati yao nao wanaliita jambo hilo ni Roho ya Mungu. Mara nyingine tena tunaona mwanadamu akimwambia Mungu, badala ya Mungu kumwambia mwanadamu.

Sasa huenda ukatamani kunikemea papa hapa kwa yale niliyosema. Vema. Wao wanajiita Wapentekoste na Injili kamili. Hebu na walithibitishe jambo hilo. Wakati wa Pentekoste moto ulishuka katika wingu na kujigawanya juu ya kila mmoja wao kama ulimi, na ukamshukia kila mmoja wao. Moto uko wapi? Walinena kwa lugha wakati wa Pentekoste na watu waliosikiliza walielewa. Jambo hilo liko wapi? Kundi lote la waaminio lilitenda kama jamaa moja. Wapentekoste wamegawanyika vibaya sana kama kundi lolote katika historia. Hakuna mtu aliyewahi kujiunga na kanisa la hapo mwanzoni ila tu wale Mungu aliowaongeza. Wana mbuzi wengi sana miongoni mwao kama wo wote wale. Wao wanadai kuwa wa Injili kamili lakini hawawezi kuthibitisha jambo hilo. Makanisa yao yamekosa nguvu kama mengine yo yote. Kama wao ndio Injili kamili basi afadhali tukubali Biblia ilikosea wakati inapoelezea walivyokuwa watu wa

Injili kamili wakati wa Pentekoste. Wao wanaimba, "Kumekuweko na badiliko kubwa ndani yangu." Wanasema kweli. Lakini hilo badiliko halijawa kwa manufaa yao.

Ni wakati wa kumrudia Mungu. Wana jina kwamba wanaishi lakini wamekufa. Lugha si thibitisho la uamsho. Ni ushahidi wa mauti. Lugha zilitangaza thibitisho ya kwamba sherehe za dini ya Wayahudi zilikuwa zimekwisha, kwamba majira mapya yalikuwa yameanza. Lugha leo zinashusha pazia juu ya nyakati za kanisa la Mataifa na Injili inawarudia Wayahudi. Watu wananena kuhusu lugha zikitangulia ufufuo mkubwa wa Kiroho. Wamechelewa. Ukweli ni kwamba zinaandika kumalizika kwa mawazo yote ya mwanadamu, taratibu na falme, na ufalme wa Mungu unafunguliwa mlango. Amkeni watu wa Mungu. Amkeni.

Kama hudhani hili ni kweli, sikiliza tu hili. Kote ulimwenguni katika makundi yote mawili ya Kipentekoste na makundi ya kanuni wanawakusanya pamoja wafanyabiashara. Wamevamia mimbara bila kuwa na wito wa Mungu. Wanajiita wavuvi wa watu na waanzilishi wa kazi za Mungu, nao wanasema ya kwamba ile huduma ya vipawa ya Waefeso 4:10-13 ambayo Mungu aliipa kanisa imeshindwa, kwa hiyo wao wanaingilia kati. Hapa tuko katikati ya kutimizwa kwa unabii, unaoitwa maasi ya Kora, na hata hawajui ya kwamba wao wameyatimiza. Wao wanaendelea bila kufikiri wakihubiri ujuzi badala ya ile kweli. Mungu na awahurumie. Jalia macho yao yafunguliwe kabla ya kuchelewa sana. Loo, nisikilizeni. Ni wakati gani fahari ya pesa, uongozi wa binadamu, uwezo wa kibiashara, ama ujasiri wa akili tupu zilimstahilisha mtu apate uongozi wa kiroho, ama kutoa uzito wo wote kwenye Neno la Mungu? Na wakati kwa njia yo yote mali ama sifa za kibinadamu zilipoanza kuonyesha kama njia ambayo kwayo Mungu hutenda kazi badala ya Roho Mtakatifu PEKE YAKE, basi tunapigana na Mungu, hatumpiganii Yeye.

Sasa nataka jambo hili liwekwe kwenye kumbukumbu papa hapa. Mimi sizungumzi dhidi ya wazee kanisani. La bwana. Na mzee huyo anaweza kuwa maskini kama mtu ye yote alivyopata kuwa maskini, ama awe mtu tajiri kuliko wote duniani mradi tu yeye ni mzee moyoni na katika matendo. Singesita kumwekea mikono mtu ye yote aliye na sifa halisi za Kiroho kama mzee ama shemasi bila kujali mali zake na cheo chake miongoni mwa watu. Lakini unapoona mfumo wa fedha ama wa watu kanisani ambao unawagawanya watu kwa namna yote ile_huo si wa Mungu. Ni ishara nyingine ya wakati katika wakati huu tunaoishi wa Laodikia ulio tajiri kimwili lakini umefilisika Kiroho.

"Ninajua umasikini wako." Je! ulitambua ya kwamba umaskini wao unahusiana na sinagogi la Shetani katika aya ile ile? Naam, ni madhehebu yaliyo tajiri na yenye nguvu na ambayo yana mali na daima yanawasukumia nje watu wachache maskini wanaomtumikia Mungu. Wakati Roho wa Mungu anapotenda kazi katika mioyo ya wanadamu, ni akina nani wanaoacha majumba na mali? Lile kundi dogo daima hushindwa na madhehebu makubwa. Na watu huenda wapi basi? Wao wanaabudu manyumbani, kwenye majengo ya maghala ya kale, na vyumba vya chini ya nyumba, kama tu walivyofanya wakati walipoenda kwenye yale mapango ya kuzikia.

Watu hawa walikuwa maskini katika mali ya ulimwengu huu. Hakika. Lakini walikuwa matajiri katika Roho.

*"Najua matukano yao."* Sasa wazo hapa si kwamba hawa waongo wanamtukana Mungu, ingawa hilo ni wazi. Lakini wanalitukana kanisa la kweli. Daima ndivyo ilivyo. Wayahudi wa Yerusalemu walilikufuru kanisa hapo mwanzo. Waabudu miungu wa Mataifa walifanya vivyo hivyo. Kama mtu ye yote atanenwa mabaya, itakuwa sikuzote ni ule mzao wa kweli. Katika siku za Nero Wakristo walilaumiwa kwa kila msiba_hata kwa kule kuteketezwa kwa Rumi. Katika nchi za ukomunisti kundi hilo dogo daima ndilo la kwanza kuangamizwa ingawa kwa kweli ni dogo sana kwa ukubwa. Ingawa Wakristo ni watu wazuri na waaminifu, ambao hutenda tu yaliyo mema, daima watateswa kusudi hatimaye wapate kuangamizwa kimwili.

Sababu ya jambo hili kuwa hivi, ni kwa sababu wao ni kemeo kwa wasio wacha Mungu. Kama vile kidole chenye kidonda wao wanaonekana dhahiri mbele ya walio waovu. Na ingawa wenye haki hawakusudii madhara yo yote kwa walio waovu ila wanataka kutenda tu mema, kila wakati wanajikuta wamefitinika kama vile ilivyokuwa kati ya Yohana Mbatizaji na Herode. Kwa maana Yohana hakutaka kumdhuru Herode wala mkewe bali kuwaokoa na hasira ya Mungu. Hili si kwamba tu lilieleweka vibaya kabisa na kupingwa kata kata, lakini Yohana aliuawa kwa sababu ya jambo hilo. Na kwa mema yote yale watu wa Mungu wanayofanya, bado wanaaibishwa hadharani na kuuawa. Hakika hapana shaka kuna nguvu mbaya nyuma ya watu ambao wangekosa dhamira namna hiyo hivi kwamba wangerudishia mabaya kwa wale waliowatenda mema. Naam, kuna nguvu kama hiyo. Ni Shetani. Jibu liko katika aya inayofuata.

**MIAKA KUMI YA DHIKI**

Ufunuo 2:10

> *"Usiogope mambo yatakayokupata; tazama, huyo ibilisi atawatupa baadhi yenu gerezani ili mjaribiwe, nanyi mtakuwa na dhiki siku kumi; uwe mwaminifu hata kufa, nami nitakupa taji ya uzima"*

Kila wakati Bwana anapoyatumia maneno hayo, "Usiogope," kuna mapambano karibuni ambayo ni ya hatari kuu na mateso na hasara. Sasa Yeye hasemi waziwazi, na kwa kifupi, "Dhiki inakuja." Hilo lingemwogopesha mtu. Lakini kama mama aliye karibu na kuzima taa anavyomwambia mtoto wake kwa upole asije akaogopa, "Sasa usiogope, kwa maana taa itazima na kutakuwa na giza. Lakini kumbukeni ya kwamba nipo hapa pamoja nanyi." Kwa hiyo Yeye anasema, "Msimwogope mwanadamu ama yale anayoweza kuwafanyia. Mimi niko pamoja nanyi, na neema Yangu inawatosha. Mnapopitia katika maji, hayatawazamisha. Hata katika mauti hamshindwi. Ninyi ni zaidi ya washindi."

Yule mtume mashuhuri, Paulo, alijua kutokana na uzoefu wa mambo ukweli wa maneno hayo na akaandika katika Warumi 8:35-59,

> *"Ni nani atakayetutenga na upendo wa Kristo? Je! ni dhiki, au shida, au adha, au njaa, au uchi, au hatari, au upanga?*
>
> *Kama ilivyoandikwa, ya kwamba, Kwa ajili Yako tunauawa mchana kutwa; tumehesabiwa kuwa kama kondoo wa kuchinjwa.*
>
> *Lakini katika mambo hayo yote tunashinda, na zaidi ya kushinda, kwa yeye aliyetupenda.*
>
> *Kwa maana nimekwisha kujua hakika ya kwamba, wala mauti, wala uzima, wala malaika, wala wenye mamlaka, wala yaliyopo, wala yatakayokuwapo,*
>
> *Wala wenye uwezo, wala yaliyo juu, wala yaliyo chini, wala kiumbe kinginecho chote hakitaweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu."*

La, hatupaswi kuogopa. Upendo Wake huondoa hofu yote.

Sasa angalia yale Yeye anayosema, "huyo ibilisi atawatupa baadhi yenu gerezani ili mjaribiwe." Wayahudi walikuwa wakifanya jambo hilo papo hapo. Makuhani wa kipagani walikuwa wakifanya jambo hilo papo hapo. Maliwali waliojaribu kujipendekeza kwa watu kwa sababu hao watu walifurahishwa na uwanja wa michezo, waliwatupa Wakristo kwa nguvu wakafe kwa maelfu, wakiwaangamiza kwa simba na wapiganaji. Ibilisi ana uhusiano gani na jambo hili? Kwa nini kumlaumu? A-ha, naam, lakini ni chuki ya ibilisi ndiyo iliyo nyuma ya jambo hilo lote. Yeye yuko nyuma ya yote kwa kuwa anamchukia Mungu. Jambo ambalo Mungu anataka kufanya, Shetani lazima ajaribu kuliharibu. Lakini angalia. Hapa kuna mwangaza fulani. Kama Shetani yuko nyuma ya Wayahudi wanaowakokota Wakristo kuwapeleka mahakamani, basi Wayahudi wale si wa dini ya Mungu bali ya ibilisi. Kusanyiko lao pia ni la sinagogi la Shetani. Na kama Kanisa Katoliki la Kirumi liliua umati wa waamini katika zile Nyakati za Giza, naam na katika nyakati zote, basi wao ni wa ibilisi na ni wa Shetani, pia.

Na kama unafikiri jambo hili linastusha, hebu ngoja tu mpaka unabii wa Ufu. 13 utimizwe. Kwa kweli linastaajabisha sana ya kwamba Marekani iko kwenye sura hiyo. Namba yenyewe kumi na tatu tu ni ishara ya taifa hili. Lilianza na koloni kumi na tatu. Bendera yake ina nyota kumi na tatu na milia kumi na mitatu. Na hayo hapo ndiyo yatakayompata katika hiyo sura ya kumi na tatu. Katika picha hii inayozungumzwa katika sura hii kutaonekana uovu wote wa yule mnyama aliyemtangulia. Kama vile yule mnyama alivyoinuka kwenye lile Baraza la Nikea, vivyo hivyo sanamu hiyo itatokea kwenye Baraza la Makanisa Ulimwenguni pamoja na nguvu zote chafu na za Kishetani kuelekeza hasira ya ibilisi juu ya mzabibu wa kweli wa Mungu. Itakuwa ni kurudia matendo ya ujanja wote wa kiibilisi na ukatili.

Wale wanaowashambulia wanyenyekevu wa Mungu na kuwadhihaki na kuwaangamiza_waache wafanye hivyo. Na kufanya hivyo watafanya. Na yote katika Jina la Mungu na dini. Lakini wao wanasema uongo. Wao si wa Mungu. Wao ni wa baba yao, ibilisi. Wao, kwa matendo yao dhidi ya watu WO WOTE, wanajionyesha jinsi walivyo. Acha waunde madhehebu na kulitenga lile kundi dogo. Wao hawafanyi lo lote ila wanawaonyesha watu wote zaidi ya kwamba wao ni wa ibilisi. Wao ni mzabibu wa uongo_mzabibu ambao huua. Chuki yao inathibitisha wao ni nani. Wao ni kanisa la Wanikolai wapinga-Kristo.

*"Watatupwa gerezani."* Naam, wao wanakokotwa kupelekwa mahakamani na kushtakiwa kwa uongo na kuhukumiwa na kutiwa gerezani. Na bila shaka yote yanafanywa katika jina la dini na uungwana na kwa ukatili wa dhamira safi. Yote yamefanywa kwa kusudi zuri. Hilo linanifanya niwazie juu ya Mahakama Kuu kukataza maombi na kusomwa kwa Biblia shuleni. Ni nani aliye nyuma yake? Ni Shetani. Ni mlipuko mwingine wa hasira dhidi ya Mungu.

*"Nanyi mtakuwa na dhiki siku kumi."* Huu hapa unabii. Na pamoja nao kuna njia ya kuamua muda Wakati wa Smirna utakaodumu. Diokleshan, mfalme mkatili kuliko wafalme wote, alianzisha kampeni ya kutisha dhidi ya watakatifu wa Mungu, hivi kwamba isingalikuwa ni kwa ajili ya rehema za Mungu ingeliwaangamiza waamini wote. Ilikuwa ndiyo yenye umwagaji wa damu sana kuliko zote katika historia na ilidumu miaka kumi (zile siku kumi za Ufu. 2:10b) kutoka 302 hadi 312.

*"Uwe mwaminifu hata kufa."* Yeye hasemi uwe mwaminifu mpaka kufikia kufa, lakini mpaka unakufa. Huenda ikakubidi kutia muhuri ushuhuda wako kwa damu yako. Maelfu, naam mamilioni, wamekufa katika

nyakati zote. Walikufa katika imani. Kama vile Antipa, yule shahidi mwaminifu, wao hawakuyashikilia maisha yao kuwa ni ya thamani hata kufa. Mara nyingi tunafikiri ya kwamba lingekuwa karibuni ni jambo lisilowezekana kuwa mfia imani. Lakini thubutu kukumbuka ya kwamba ile imani tunayotumia kila siku kushinda katika Kristo Yesu ndiyo imani ile ile inayowashikilia akina Polikapu na wafia imani wote. Imani kuu itatoa neema kuu kwa ajili ya ile saa kuu. Mungu na abarikiwe milele!

*"Nami nitakupa taji ya uzima."* Kwa kuwa si hata kikombe cha maji baridi kinachotolewa katika Jina la Bwana kinakosa kupokea thawabu, thawabu yake yeye anayeyatoa maisha yake kama mfia imani kwa ajili ya Jina la Bwana Yesu itakuwa kubwa jinsi gani. Labda tunaweza kupata wazo dogo kama tukilinganisha taji hii na taji inayovaliwa katika mashindano ya mbio.

Katika I Wakorintho 9:24, Paulo anasema,

> *"Je! hamjui, ya kuwa wale washindanao kwa kupiga mbio, hupiga mbio wote, lakini apokeaye tuzo ni mmoja? Pigeni mbio namna hiyo, ili mpate."*

Taji iliyotolewa kwa mshindi wa mbio za Olimpiki ilikuwa ni shada la matawi ya mizeitumi. Lakini taji inayotajwa hapa katika Ufunuo, inayotolewa kwa mfia imani, ni taji ya kifalme. Yesu anaiita taji ya uzima. Taji hiyo moja ni kwa wale ambao wameshinda; hiyo nyingine ni kwa wale ambao wametoa. Taji zote mbili haziharibiki. Hazitaharibika. Washindi wa mbio za ulimwengu za maisha karibuni watapoteza furaha ya mashabiki wa ulimwengu. Utukufu wao utakwisha. Lakini wale wanaoyatoa maisha yao kwa ajili ya Mungu, aidha kwa kushindana kila siku ama kwa kumwaga damu yao kama dhabihu ya kuyakamilisha maisha yao watapewa taji ya uzima.

Wakati mdogo sana hutumiwa katika kutaabika kwa thawabu za milele za Mungu. Malipo ya Mungu hayatiliwi maanani sana. Kama tunaamini katika ukweli wa kufufuka kwa mwili, na ufalme wa milele unaoonekana, basi tunapaswa kuweka mbinguni zile hazina nzuri ambazo ziko kwa ajili ya watakatifu waaminifu.

**THAWABU KWA KUSHINDA**

Ufunuo 2:11,

> *"Yeye aliye na sikio na alisikie Neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa. Yeye ashindaye hatapatikana na madhara ya mauti ya pili."*

Sasa, mara nyingine tena Roho ananena na nyakati zote. Ujumbe huu ni wa kutufariji leo kama vile ulivyowafariji ndugu zetu wa nyakati zile nyingine. Naye anatwambia ya kwamba mauti ya pili haitatudhuru.

Sote tunajua ya kwamba mauti ya pili ni lile ziwa la moto.

Ufunuo 20:14,

> *"Mauti na Kuzimu zikatupwa katika lile ziwa la moto. Hii ndiyo mauti ya pili."*

Bila shaka hiyo inamaanisha hao wote waliokuwa mle, walitupwa katika ziwa la moto. Sasa basi, ninataka kuleta jambo fulani hapa kwa ajili yenu. Bila shaka litawafanya watu kusema mambo juu ya fundisho langu la kigeni.

Lakini ninasimama hapa juu ya mamlaka ya Neno la Mungu na kukana ya kwamba asiyeamini anaenda kwenye kuzimu ya milele na kuteketezwa huko milele. Kwanza, kuzimu, ama ziwa la moto, ama vyo vyote unavyotaka kuliita si la milele. Linaweza kuwa wakati lilikuwa na mwanzo? Katika Mt. 25:41, inasema ya kwamba *"moto wa milele uliwekewa tayari ibilisi na malaika zake."* Sasa kama uliwekewa tayari, basi haukuwa usio na mwanzo. Kama ulikuwa na mwanzo, basi hauwezi kuwa ni wa milele. Bila shaka huenda ukajikwaa juu ya wazo la neno 'milele.' Lakini neno hilo linamaanisha "toka nyakati hadi nyakati" na lina maana tofauti zinazoambatana nalo. Katika I Sam. 3:13-14, Mungu alimwambia Samweli ya kwamba angeihukumu nyumba ya Eli milele, na ya kwamba hawangetoa dhabihu nyingine "milele" kama makuhani Wake. Na katika 2 Waf. 2:27, Sulemani anautupilia mbali ukoo wa Eli kutoka katika ukuhani. Hivyo vilikuwa kitu kama vizazi vinne baadaye. Sasa unaweza kuona ya kwamba "daima" halilingani na kile kilicho cha "milele", ama kile kisichokuwa na mwanzo wala mwisho. Hapa katika kisa hiki neno milele linamaanisha "kufikia mahali pa kutoweka." Hilo ndilo lililotukia. Walitoweka.

Angalia neno, "maangamizi" kwenye II Thes. 1:9,

> *"Watakaoadhibiwa kwa maangamizi ya milele."*

Katika Kiyunani "maangamizi" kweli linamaanisha kuharibu kabisa. Na neno, "maangamizi", HALIMAANISHI kuharibu. Sasa "kuharibu" kunamaanisha kitu fulani kinachoendelea na kuendelea katika kuharibika. Kwa hiyo kuharibu milele kunaweza kuwa na maana gani? Hakumaanishi kuendelea kuharibu, la

sivyo hilo lingelifanya neno "kuharibu", kuchukua mahali pa "maangamizi." Linamaanisha kuharibu mpaka kiishe. Kukimaliza

Unaweza ukashangaa sasa, ni wakati gani unapoweza kutumia neno, "milele," na usilitumie jinsi ambavyo tumefundishwa. Hilo ni rahisi. Wakati litumikapo kumhusu Mungu linamaanisha kuwa bila mwanzo wala mwisho, na kudumu daima na bila kikomo. Na wakati unaponena juu ya uzima wa milele unawazia niani mwako kile ambacho ni uzima wa Mungu. "Huu ndio ushuhuda, ya kwamba Mungu ametupa uzima wa milele, na uzima huo umo katika Mwanawe. Yeye aliye na Mwana yuna uzima." Sasa basi, wana wa Mungu tu ndio walio na uzima wa milele, ule ambao haukuwa na mwanzo, lakini ulikuwako daima. Hiyo ni kweli. Una kitu fulani ndani yako sasa hivi ambacho ni cha milele_ bila mwanzo wala mwisho. Ni Roho wa Mungu. Ni sehemu ya Mungu Mwenyewe. Ni uzima wa Mungu.

Sasa kama mwenye dhambi ataenda kuzimu na halafu ateseke jinsi wewe unavyoenda mbinguni na kufurahia mbingu, basi tayari yeye ana uzima wa namna ile ile ulio nao wewe.

Vema, basi huenda kukawa na wale wanaosema uzima wa milele unaonyesha ustawi wa watoto wa Mungu. Kustawi kwao na halafu furaha yao ndivyo vilivyo hatarini. Kwa upande mwingine mwenye dhambi anaenda kwenye adhabu yake, hivi kwamba tunaweza kurahisisha mauti ya pili kuwa kitu tu cha adhabu na mahali fulani. Uzima wa milele unamaanisha mbinguni, na adhabu ya milele inamaanisha kuzimu. Ungeshangazwa na watu ambao wametukuzwa sana kama wanatheolojia ambao wameamini jambo hilo. Lakini unajua hilo linafanya nini? Linaufanya uzima wa milele kuwa tu ni jambo la kijiografia badala ya Mtu. Uzima wa milele ni Mungu, —Bwana Yesu Kristo. Jinsi mtu ye yote angeweza kuamini jambo kama hilo, ya kwamba uzima wa milele ni mahali fulani tu, ni zaidi ya ninavyojua. Linanifanya kuduwaa nikiliwazia

La bwana. Kuna aina moja tu ya uzima wa milele. Mungu anao. Kama tuna Mungu, tuna uzima wa milele ndani Yake na kupitia Kwake.

Kwa hiyo unaona, hilo neno milele, ama daima, linaweza kutumiwa katika njia mbalimbali, lakini wakati linapotumiwa kwa Mungu, Yeye akiwa jinsi alivyo, lina maana moja. Ni kudumu kwa Mungu. Huwezi kulitumia namna hiyo kwa kitu kingine chochote. Mungu pekee ndiye wa milele, na kwa sababu Yeye yu hai, tunaishi pamoja Naye.

Sasa mtu yeyote asiseme ya kwamba siamini katika ziwa la moto na adhabu. Ninaamini. Sijui litadumu muda gani, lakini hatimaye litaondolewa. Katika Ufu. 21:8, inasema ya kwamba hao wenye dhambi waliotajwa watakuwa na sehemu yao katika ziwa la moto. Lakini tafsiri ya kweli ya neno si "sehemu" bali ni "wakati." Mnaona, hapo umelipata.

Kwa hiyo walio waovu watatupwa katika kuzimu (Jehanum ama kaburini) na kuzimu katika ziwa la moto. Kutengwa na Mungu. Hilo litakuwa ni jambo la kutisha jinsi gani.

Bali kwa wenye haki haitakuwa hivyo. Haiwapasi kuogopa. Wamekombolewa na Mungu. Wako kifuani Mwake. Wao ndio washindi. Naye ni nani ashindaye? Yeye aaminiye ya kwamba Yesu ni Kristo.

Ni kwa nini huyu mshindi, huyu mwamini aepuke, na aingie katika milki ya uzima wa milele na kipeo cha raha? Kwa sababu Yesu alilipa gharama kutukomboa na dhambi. Yeye alijaza pengo la utengano, nasi tuliokuwa mbali sasa tumekaribishwa kwa damu.

Nao kamwe hawataingia hukumuni. Hawatakuwa kamwe katika lile ziwa la moto. Hawawezi kamwe kupotea kwa kuwa hatapoteza hata mmoja wao. Hakuna hata mmoja wa waliokombolewa atakayekuwa mahali popote isipokuwa mahali Yesu alipo.

Unajua ni kwa nini hivyo? Nitawaelezea jambo hilo. Nina mvulana mdogo, Joseph. Yeye ni sehemu yangu, haidhuru nini kitatendeka. Kama ningekuwa mtu tajiri, kibaya zaidi ningeweza kufanya ni kumwondolea urithi, lakini hakuna kitu ambacho ninaweza kufanya kumkana. Siwezi kwa sababu yeye ni sehemu yangu. Hapa, hebu tupimwe damu. Hebu na tulinganishe damu yake na yangu. Itathibitisha ya kwamba Joseph ni mwanangu. Yeye ni wangu.

Ni jaribio la damu ndilo linaloonyesha kama wewe ni wa Mungu au la.

Siwezi kujizuia kufikiria juu ya wakati nilipokuwa nikisimamia ng'ombe wa gredi wa Hereford huko Colorado. Tulikuwa tunawaleta hao ng'ombe wapate kuchunguzwa na serikali kama tulitaka walishwe kwenye ranchi ya serikali. Lakini wasingeruhusu hata mnyama mmoja asiyekuwa na kipande cha kuonyesha damu yake kwenye sikio lake. Kipande hicho kilionyesha ya kwamba yeye alikuwa ni wa gredi. Walinzi waliowachunguza hawakuangalia hata mara moja chapa yao. Waliangalia tu kile kipande kuona ya kwamba ile damu ilikuwa damu halisi. Haleluya. Kama ni damu sahihi, haina budi kuwa sahihi.

Unajua Mungu aliangalia chini na kutangaza, "Nafsi itendayo dhambi, itakufa. Imetengwa na Mimi. Hawezi kunikaribia Mimi." Tunajua ya kwamba sote tumetenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu. Hiyo ilimaanisha ya kwamba wote walikufa, wote walitengwa, na siku moja wakati ungekuja

ambapo hata sehemu hiyo ndogo sana ya uhai itaondolewa na yote yatakwisha. Lakini Mungu katika upendo, alichukua mnyama na kuutoa uhai wake badala ya uhai wa mwenye dhambi.

Katika Agano la Kale mwenye dhambi alimleta mwanakondoo. Akaweka mkono wake juu ya mwana-kondoo huyo huku kuhani anakata koo la yule mwana-kondoo. Alihisi kule kutoka kwa damu na akasikia kule kulia. Akasikia mwili ukijinyosha ukifa. Aliona moshi wa damu iliyonyunyizwa ukipaa kwa Mungu. Alijua huyo mwana-kondoo amepachukua mahali pake. Alijua ya kwamba uhai wa huyo mwana-kondoo ulikuwa umetolewa badala ya wa kwake. Lakini uhai wa mwana-kondoo huyo ulikuwa ni uhai wa mnyama wala haukuweza kumrudia mwenye dhambi na kumfanya msafi. Kwa hiyo akaondoka akiwa na shauku ile ile ya kutenda dhambi. Angeondoka akiwa na dhambi moyoni mwake, na kurudi na kutoa dhabihu kwa ajili ya jambo lile lile mwaka mmoja baadaye.

Lakini katika Agano Jipya sivyo ilivyo. Mwana-Kondoo wetu anayekufa ni Mwana wa Mungu Ambaye alitoa damu Yake kuwa fidia kwa ajili ya wengi. Kwa imani tunatembea na kuweka mikono yetu juu ya Mwana-Kondoo huyo_tunamwona akiwa na jeraha zilizojaa damu, mgongo uliojeruhiwa, na miiba mikali sana ikiumbua paji Lake_tunahisi maumizu Yake na kumsikia akilia, “Mungu Wangu, Mungu Wangu, mbona umeniacha?” Na ni jambo gani lililotukia? Uhai ulioiacha chembechembe hiyo ya damu iliyovunjwa-vunjwa ulimrudia mwenye dhambi aliyetubu. Uhai uliokuwa ndani Yake ulirudi juu yetu. Tunarudi pasipo na tamaa tena ya kutenda dhambi, na sasa tuna chuki kwa matendo na tamaa za mwili.

Tuangalie. Uhai wetu ni nini? Ni chembechembe ndogo moja tu iliyotoka kwa baba yetu. Mwanamke hana ile sehemu nyekundu ya damu. Yeye hutoa yai; yeye ni chombo cha kuatamia. Bali damu hutoka kwa mwanamume. Hiyo ndiyo sababu mwanamke huchukua jina la mwanamume. Watoto wanachukua jina lake. Mama ni chombo cha kuatamia watoto anaomzalia.

Hilo ndilo lililotukia kwa ajili ya ukombozi wetu. Roho Mtakatifu alimjia Mariamu naye akamzaa Mwana na kumwita, Yesu. Yule Muumba mkuu alishuka na akawa dhabihu kwa ajili ya dhambi zetu. Damu yake ilikuwa ni damu ya Mungu. Hivyo ndivyo ilivyokuwa hasa. Hiyo damu ya Mungu ilimwagwa na Roho akamwacha wakati alipokufa kwa uchungu. Ndipo UHAI ULE ULE (ROHO) ukarudi kukaa ndani ya mwenye dhambi aliyetubu na kumweka huru. Mwenye dhambi huyo hakurudi mwaka baada ya mwaka, dhabihu baada ya dhabihu, kwa maana hapakuwepo na haja. Kwa dhabihu MOJA, mara moja tu yeye amewekwa huru kutoka katika utawala wa dhambi, naye ameupokea uzima wa Kristo ambapo yeye anatawala kwa ushindi juu ya dhambi, ulimwengu, mwili na ibilisi.

Mungu alifanya hivyo. Yeye alifanya yote. Yeye aliulilia ulimwengu uliolaaniwa katika dhambi, “Nitawapa ishara. Bikira atachukua mimba. Bikira atachukua mimba na kuzaa Mwana. Hiyo itakuwa ndiyo ishara yenu. Itakuwa ni ishara ya milele. Kile atakachozaa kitakuwa Imanueli, Mungu pamoja nasi.”

Mungu alishuka katika chembechembe ya damu, si kwa kupitia kwa mwanadamu, lakini kwa Roho Mtakatifu, na katika tumbo hilo la uzazi la bikira maskani ilijengwa kwa kusudi la mauti. Mzao wa mwanamke ulikuja ili Yeye apate kuchubuliwa kusudi atuletee wokovu wetu. Wakati Roho Mtakatifu alipomjilia Mariamu, Yeye aliumba ndani ya tumbo lake la uzazi chembechembe ile ambayo ingeongezeka na kuwa mwili wa Bwana wetu. Seli hiyo iliumbwa. Ilikuwa ndiyo Mwanzo wa Kuumba kwa Mungu. Huyo Ndiye Yesu. Na huyo Mtakatifu alijazwa na damu Takatifu, yaani ni damu ya Mungu. Maskani hiyo ikaja kuzaliwa. Akakua akawa mtu mzima. Akaenda Yordani na hapo hiyo Dhabihu ikaoshwa na Yohana katika mto unaoitwa Yordani. Wakati dhabihu hiyo iliyokubalika ilipoinuka kutoka majini, Mungu alikuja akaishi ndani Yake, akimjaza kwa Roho bila kipimo. Na wakati alipokufa na kumwaga damu Yake, ule uzima mkamilifu wa Mungu ulitolewa umrudie mwenye dhambi ambaye angemkubali Kristo kama Mwokozi wake.

Loo, jinsi inavyoshangaza. Yehova, aliyezaliwa akilia juu ya lundo la samadi. Yehova alizaliwa katika hori la majani. Hiyo hapo ishara yako ya milele kwa wenye majivuno na wenye kiburi, na wenye elimu bandia, ambao wamebuni theolojia yao wenyewe na kukana kweli ya Mungu. Yehova Mungu, mtoto mchanga anayelia katika hori linalonuka. Halafu tunafikiri tuna haki ya kuwa na majivuno, huku tukiinua juu pua zetu, tukilaumu na kufanya kana kwamba tulikuwa watu mashuhuri. Hii hapa ishara yako halisi. Hii ndiyo ya kweli. Yehova, akicheza kama mvulana. Yehova akifanya kazi katika duka la seremala. Yehova akiosha miguu ya wavuvi.

“Nitawapa ishara,” alisema Mungu. “Si ishara ya ukasisi wenye ukosi mweupe. Si ishara ya utajiri na mamlaka. Hakuna kitu katika ishara hii ambacho mtakipenda, ama mtakachofikiria kinafaa. Bali ni ishara ya milele. Ni ishara iliyo kuu kuliko zote.” Yehova akisimama kwenye behewa amechubuliwa na kutokwa na damu akiwa na miiba kwenye paji la uso Wake na mate aliyotemewa usoni, akidhihakiwa na kufanywa si kitu. Yehova akidhihakiwa na kukataliwa, ameangikwa uchi msalabani, huku wanafiki wakimfanyia mzaha na kumsai ashuke msalabani. Yehova akifa. Yehova akiomba na hakuna kitu kinachotendeka. Ndipo Yehova akafa. Hiyo ndiyo ishara kwa watu wote sasa. Hakuna nyingine kama hiyo. Ndiyo iliyo kuu.

Ndipo giza likaja juu ya nchi. Walimweka kaburini. Hapo akalala hizo siku tatu usiku na mchana mpaka tetemeko la nchi lilipolivunja giza la usiku Naye akafufuka. Yehova akafufuka. Yehova akapaa juu. Ndipo Yehova akarudi kuishi ndani ya kanisa Lake. Yehova akarudi kwa upepo wa nguvu ukienda kasi na ndimi

za moto. Yehova akarudi kuja kutembea kati ya kanisa Lake na kuwatia nguvu watu Wake. Mara nyingine tena Yehova alikuja, na wakati huu kukaa katika watu Wake. Na tena Yehova huwaponya wagonjwa, huwafufua wafu na kujidhihirisha kwa Roho. Yehova alirudi, akinena kwa lugha, na kutoa jibu katika tafsiri.

Yehova alishuka na kumwinua kahaba asitende dhambi tena. Alishuka kuja kwa mlevi aliyejaa nzi usoni mwake akiwa amelala amezirai kwenye handaki. Naam, Yehova alikuja kujidhihirisha katika mwili na kujidhihirisha kwa mwili. Yehova alikuja_Mungu ndani yetu, tumaini la utukufu.

Naam, Yesu alikuja na kumwaga damu Yake na kumweka mfungwa huru. Yeye alikuja na kuwakomboa kondoo Wake waliopotea. Aliwapa uzima wa milele nao hawataangamia. Hatapoteza hata mmoja wao, bali atawafufua katika siku ya mwisho.

Haleluya, mauti ya pili haiwezi kuwaumiza. Haina nguvu juu yao. Kwa kuwa wao ni wa Mwana-Kondoo nao wanamfuata kila aendako.

**ROHO MTAKATIFU KATIKA KILA WAKATI**

Ufunuo 2:11,

*"Yeye aliye na sikio, na alisikie Neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa."*

Hakuna wakati mmoja wa kanisa ambapo aya hii haikutajwa. Kila wakati una onyo lile lile kwa watu wa kila wakati. "Yeye aliye na sikio, na alisikie Neno hili ambalo Roho anasema." Lakini haiwezekani kabisa kwa watu wote kusikia yale ambayo Roho anaziambia nyakati mbalimbali.

I Wakorintho 2:6-16,

*"Walakini iko hekima tusemayo ya wakamilifu; ila si hekima ya dunia hii, wala ya hao wanaoitawala dunia hii, wanaobatilika;*

*Bali twanena hekima ya Mungu katika siri, ile hekima iliyofichwa, ambayo Mungu aliazimu tangu milele, kwa utukufu wetu;*

*Ambayo wenye kuitawala dunia hii hawaijui hata mmoja; maana kama wangaliijua, wasingalimsulibisha Bwana wa utukufu;*

*Lakini, kama ilivyoandikwa, mambo ambayo jicho halikuyaona wala sikio halikuyasikia, (wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu,) mambo ambayo Mungu aliwaandalia wampendao.*

*Lakini Mungu ametufunulia sisi hayo kwa Roho Wake. Maana Roho huchunguza yote, hata mafumbo ya Mungu.*

*Maana ni nani katika binadamu ayajuaye mambo ya binadamu ila roho ya binadamu iliyo ndani yake? Vivyo hivyo na mambo ya Mungu hakuna ayafahamuye ila Roho wa Mungu.*

*Lakini sisi hatukuipokea roho ya dunia, bali Roho atokaye kwa Mungu, makusudi tupate kuyajua tuliyokirimiwa bure na Mungu.*

*Nayo twayanena, si kwa maneno yanayofundishwa kwa hekima ya kibinadamu, bali yanayofundishwa na Roho Mtakatifu, tukiyafasiri mambo ya rohoni kwa maneno ya rohoni.*

*Basi mwanadamu wa tabia ya asili hayapokei mambo ya Roho wa Mungu; maana kwake huyo ni upuzi, wala hawezi kuyafahamu, kwa kuwa yatambulikana kwa jinsi ya Rohoni.*

*Lakini mtu wa Rohoni huyatambua yote, wala yeye hatambuliwi na mtu.*

*Maana, Ni nani aliyeifahamu nia ya Bwana, amwelimishe? Lakini sisi tunayo nia ya Kristo."*

Mathayo 13:13-16,

*"Kwa sababu hii nasema nao kwa mifano; kwa kuwa wakitazama hawaoni, na wakisikia hawasikii, wala kuelewa.*

*Na neno la nabii Isaya linatimia kwao, likisema, Kusikia mtasikia, wala hamtaelewa; kutazama mtatazama, wala hamtaona.*

*Maana mioyo ya watu hawa imekuwa mizito, na kwa masikio yao hawasikii vema, na macho yao wameyafumba; wasije wakati wo wote wakaona kwa macho yao, wakasikia kwa masikio yao, wakaelewa kwa mioyo yao, wakaongoka, nikawaponya.*

*Lakini, heri macho yenu, kwa kuwa yanaona; na maskio yenu, kwa kuwa yanasikia."*

Yohana 8:42-44,

> *"Yesu akawaambia, Kama Mungu angekuwa Baba yenu, mngenipenda Mimi; kwa maana nalitoka kwa Mungu, Nami nimekuja; wala sikuja kwa nafsi Yangu, bali Yeye ndiye aliyenituma.*
>
> *Mbona hamyafahamu hayo niyasemayo? ni kwa sababu ninyi hamwezi kulisikia Neno Langu.*
>
> *Ninyi ni wa baba yenu, Ibilisi, na tamaa za baba yenu ndizo mpendazo kuzitenda. Yeye alikuwa mwuaji tangu mwanzo; wala hakusimama katika kweli, kwa kuwa hamna hiyo kweli ndani yake. Asemapo uongo, husema yaliyo yake mwenyewe; kwa sababu yeye ni mwongo, na baba wa huo."*

Ni dhahiri kabisa kutokana na Maandiko haya ya kwamba hakuna mtu kwa nafsi yake anayeweza kumsikia Mungu. Uwezo huo hana budi kupewa na Mungu.

Mathayo 16:17,

> *"Yesu akajibu, akamwambia, Heri wewe Simoni Bar-yona; kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba Yangu aliye mbinguni."*

Tukiweka aya hizi pamoja tunaona ya kwamba kuna kundi moja tu la watu, na hilo ni kundi maalum sana la watu ambao wanaweza kusikia yale Roho anayosema katika kila wakati. Ni kundi moja maalumu ndilo linalopokea ufunuo kwa kila wakati. Kundi hilo ni la Mungu, kwa sababu kundi ambalo haliwezi kusikia si la Mungu. (Yohana 8:42-44.) Kundi ambalo linaweza na linasikia yale Roho anayosema na kupokea ufunuo wake ndilo kundi lile lililoelezewa habari zake katika I Kor. 2:6-16. Hao ndio walio na Roho wa Mungu. Hao ndio waliozaliwa na Mungu. Wanabatizwa katika mwili wa Bwana Yesu Kristo kwa Roho Wake. Wao wanabatizwa kwa Roho Mtakatifu.

Kufafanua zaidi yale tuliyosema hivi punde, na pia kutumia Andiko ambalo linapaswa kuwekwa mawazoni tunapozungumza juu ya ni nani aliyebatizwa na Roho Mtakatifu, tazama yale Yesu aliyosema katika Yohana 6:45,

> "Imeandikwa katika manabii, Na WOTE watakuwa wamefundishwa na Mungu."

Lakini fungua Isa. 54:13 ambapo hili limetolewa na linasema,

> *"Na watoto wako wote watafundishwa na Bwana."*

Hao WOTE wa Mungu ni WATOTO wa Mungu. Kwa hiyo jambo hilo ndio ushuhuda wa kuwa mtoto wa kweli wa Mungu, (yeye ambaye Roho amemjilia na kukaa ndani yake) ameelezwa hapa tena kama mtu aliyefundishwa Neno na Roho Mtakatifu.

Sasa unaweza kuanza kuona ni kwa nini lugha si ushahidi wa kubatizwa na Roho Mtakatifu. Haisemi katika wakati wo wote ya kwamba "yeye aliye na lugha na anene lile ambalo Roho ananena." Hilo linaweka lugha, fasiri zake, na unabii, nk. kando kama ushuhuda. Ushuhuda ni KUSIKIA yale Roho asemayo. Roho ananena. Naam, Roho anafundisha. Hivyo ndivyo Yesu alivyosema angefanya atakapokuja.

Yohana 14:26,

> *"Atawafundisha yote na kuwakumbusha yote niliyowaambia."*

Na hivyo ndivyo ilivyotukia. Hivyo ndivyo Injili zilivyoandikwa. Watu hawa walikuwa wamekumbuka mioyoni mwao kwa Roho Mtakatifu Maneno yale yale aliyosema Yesu. Hiyo ndiyo sababu Injili ni sahihi. Wao ni wakamilifu. Lakini Roho hakuwakumbusha tu mambo yote lakini aliwafundisha zaidi juu ya ile kweli waliyokuwa nayo tayari. Hivyo ndivyo Paulo alivyopokea mafunuo yake. Alisema kuhusu jambo hilo,

> *"Kwa maana, ndugu zangu, Injili hiyo niliyowahubiri, nawajulisha ya kuwa siyo ya namna ya kibinadamu.*
>
> *Kwa kuwa sikuipokea kwa mwanadamu wala sikufundishwa (na mwanadamu), bali kwa ufunuo wa Yesu Kristo."*

Wagalatia 1:11-12. Yeye alifundishwa na Roho Mtakatifu.

Siku moja wakati Yesu alipokuwa duniani, mtu fulani muhimu alikuja kumtembelea. Mtu huyu alisema, "Rabi, tunajua wewe ni mwalimu aliyetumwa kutoka kwa Mungu." Lakini utaona ya kwamba Yesu alimkatiza. Alimgeukia Nikodemo na maneno aliyonena yanaweza kufafanuliwa namna hii, "Mimi SI mwalimu. Mimi ni Mwana-Kondoo wa Sadaka kwa ajili ya dhambi. Ninafanya Kuzaliwa Upya kuwezekane

kwa Roho Yangu. Bali kuna Mmoja anayekuja ambaye ni Mwalimu. Yeye ni Roho Mtakatifu." Wakati Yesu alipokuwa duniani Yeye alikuja kama Mwana-Kondoo, na kama Nabii. Lakini wakati aliporudi juu ya kanisa kwa Roho Wake akawa Mwalimu.

Na kwa kila wakati tunasikia kweli ile ile. *"Yeye aliye na sikio na alisikie Neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa."* Lakini ni mtu aliyejazwa na Roho tu anayeweza kusikia ufunuo kwa wakati huo. Hakuna mwingine anayeweza. La bwana. Hawawezi kwa sababu hivyo ndivyo hasa Paulo alivyosema katika I Wakorintho 2:6-16.

Sasa jambo hili linapaswa kuwafanya mfurahi. Kuna fundisho la ajabu sana linalovuma ambalo linasababisha mafarakano makubwa sana na chuki. Kwa maana hapo Wapentekoste wanaposema HUNA BUDI kunena kwa lugha la sivyo hujabatizwa na Roho Mtakatifu, wao aidha wanakana ya kwamba watu wenye sifa kama akina Knox, Moody, Taylor, Goforth na wengineo hawakumpokea Roho Mtakatifu, ama wanasema ya kwamba wote walinena kwa lugha kisiri nao wala hawakujua yaliyokuwa yakitukia. Sasa hiyo si kweli. La bwana. Hilo ni kosa kubwa sana. Lugha si ishara ya kujazwa na Roho. Ni moja tu ya yale madhihirisho tisa yaliyotajwa katika I Wakorintho 12. Hakuna Maandiko yanayosema ya kwamba unampokea Roho Mtakatifu ukinena kwa lugha au kwamba unampokea Roho Mtakatifu kwa kunena kwa lugha. Lakini nasema kwamba "Baada ya wao wote kujazwa na Roho Mtakatifu walinena kwa lugha," na baadaye inasema ya kwamba walitabiri.

Leo miongoni mwa jamaa wengi inakubaliwa tu ya kwamba wote wanaodai kumpokea Roho Mtakatifu kwa kunena kwa lugha wananena kwa lugha halisi ya Kiroho. Lakini jambo hili si kweli kwa maana wengi hunena kwa lugha inayojulikana lakini chini ya ushawishi wa pepo mchafu. Sasa hebu tuseme tuko mkutanoni na watu wote wananena kwa lugha. Unawezaje kujua ni lugha gani inayotoka kwa Roho na ni ipi inayotoka kwa Ibilisi? Mimi nimekwenda miongoni mwa makafiri ambapo wachawi wao walikunywa damu kutoka kwenye fuvu la kichwa, wakanena kwa lugha na wakafasiri na kutabiri. Wanaweza hata kuandika kwa lugha.

Sasa kama lugha ndio HUO ushuhuda wa kumpokea Roho Mtakatifu, basi kila lugha itabidi iwe ni ya Mungu. Lakini imekubaliwa na watu wanaochukua lugha kuwa ni ushuhuda ya kwamba kuna lugha za uongo na za kweli kwa maana Mungu ana za kweli na ibilisi ana za uongo. Kwa hiyo swali langu ni, "Ni nani ajuaye yaliyo halisi? Ni nani aliyefahamu hiyo lugha akajua yale yaliyonenwa? Ni nani aliye na kipawa cha utambuzi kujua?" Sasa wakati tutakapopata majibu hayo tutakuwa na jambo fulani la kuendelea nalo, lakini hadi wakati huo, hatuna budi kujiuliza juu ya chanzo cha lugha hizo. Unaweza kuona papa hapa ya kwamba kama ukiunga mkono ushuhuda wa lugha na hujui yanayosemwa, itakubidi hatimaye kufikia mahali ambapo lugha zote hazina budi kuwa ni za Mungu. Jambo hilo basi lingetufanya tuamini ya kwamba ibilisi hawezi kunena kwa lugha. Hilo si kweli; la, sivyo hata kidogo. Mmishenari ye yote wa kweli akiwa huko nchi za ng'ambo anajua vizuri sana ya kwamba mapepo hunena kwa lugha, kama vile tu nijuavyo mimi kwa matukio mbalimbali niliyokuwa nayo.

Wanatheolojia wa Kipentekoste wanakubali ya kwamba hawana Andiko linalosema ya kwamba watu hunena kwa lugha wanapobatizwa kwa Roho Mtakatifu. Wanakubali ya kwamba wamelichukulia jambo hilo kutokana na matukio yaliyoandikwa katika Kitabu cha Matendo ambapo mara tatu kati ya tano watu walinena kwa lugha. Na wanasema pia bila ya Andiko lo lote ya kwamba kuna lugha za aina mbili. Moja ni lugha unayonena unapompokea Roho Mtakatifu nayo ndiyo 'ushuhuda', ambapo baadaye kama unaamini, unaweza kupokea kipawa cha kunena kwa lugha ambapo unaweza ukanena mara kwa mara.

Hata hivyo, wanasema, mara baada ya kunena kwa lugha kama ishara ya kupokea, huenda usinene tena. Mara nyingine tena tunatamani kujua ni wapi jambo hili linapatikana katika Neno. Kama halipo, basi Mungu hajalinena na ole wake yeye ambaye angeongeza kwenye Neno hilo. Lakini kuna jambo fulani katika Neno kuhusu somo lili hili ambalo wanalipuuzia kabisa. I Wakorintho 13. Inataja lugha za wanadamu na za malaika. Hizi zingekuwa lugha zinazojulikana na zisizojulikana. Wapentekoste wa kisasa wanasema ya kwamba wanaweza wao kumpokea Roho Mtakatifu wakinena katika lugha zisizojulikana ama lugha za malaika. Wameuweka mkokoteni mbele umvute farasi, kwa maana katika Matendo 2 watu walinena katika lugha halisi ambayo hata wasioamini walisikia na kufahamu.

Sasa wakati Mungu anaponyamaza afadhali tunyamaze. Lakini mahali ambapo amenena afadhali na sisi tunene, pia, na kusema yale aliyokwisha sema. Yeye alitwambia ushuhuda, ama ni jambo gani lingetukia baada ya kubatizwa na Roho Mtakatifu ilikuwa kwamba yule Mwalimu angekuja na kutufundisha kweli yote. Lakini Mwalimu huyo alikuwa ni mwalimu wa NDANI, si mwalimu wa nje. Kama Roho hakuwamo ndani, wewe hungeweza kuisikia kweli na kuipokea kwa ufunuo kama ungaliisikia kila dakika ya siku. Hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Roho anayekaa ndani katika siku za Paulo. Wale waliojazwa na Roho Mtakatifu walilisikia Neno, wakalipokea na kuishi kwalo. Wale ambao hawakuwa na Roho walilisikia tu kama watu wa kimwili, wakaweka tafsiri mbaya kwalo na wakaingia dhambini.

Katika kila wakati, (na kila wakati ni wakati wa Roho Mtakatifu kwa mwamini wa kweli)_nasema, katika kila wakati ushuhuda ulikuwa ni ule ule. Wale waliokuwa na Roho, yule Mwalimu, walilisikia lile

Neno, na huyo Roho aliyekuwa ndani yao alilichukua lile Neno na kulifundisha (akalifunua) kwao; nao walikuwa ni wa kundi lile lililomsikia yule mjumbe na ujumbe wake na kuuchukua na kuuishi.

Ninajua ni ushawishi mkubwa wa kurejea nyuma kwenye siku ya Pentekoste na pia kwenye siku ambapo Roho Mtakatifu aliposhuka katika nyuma ya Kornelio na halafu kuweka hayo matukio mawili yanayolingana kama ushuhuda wa Ubatizo wa Roho Mtakatifu. Lakini katika kila moja ya matukio hayo zile lugha zilieleweka kwa wale waliosikiliza. Hii ni mbali sana na babeli ya kisasa ya mchafuko wa mikutano ya Kipentekoste. Na kama jambo hili halitoshi kutushawishi kutupilia mbali hoja kama hizo, tutafanyaje tutakapokabiliwa na ukweli kwamba watu ambao hawajawahi kunena kwa lugha kamwe wana baadhi ya yale madhihirisho mengine manane maishani mwao, kama vile neno la hekima, upambanuzi wa roho, neno la maarifa, imani, kuponya na hata miujiza? Na maneno haya yanavutia hata na zaidi katika ukweli kwamba lugha ndiyo iliyo ndogo sana kuliko zile karama tisa; kwa hiyo wakati tunapoona watu ambao hawaneni, wala hawajapata kunena kwa lugha, wakitumia karama kuu kuliko wale wanaonena kwa lugha, hatuna budi kukanusha fundisho kama hilo kwa dhati hata kuliko ilivyowali kuwa.

Kwa hiyo unaweza kuona sasa, ya kwamba hatuwezi kuthubutu kusema yale ambayo Biblia haikusema. Wakati Maandiko yanapotufundisha ya kwamba kazi za Roho Mtakatifu, na dhihirisho la Mtu huyo Aliyebarikiwa ni kuleta kweli ya kila wakati kwa uzao wa kweli wa wakati huo, basi tunajua ya kwamba Roho hana budi kuwa anakaa ndani ya mtu huyo la sivyo hawezi kupokea kweli ya wakati huo. Amina. Hiyo ni kweli kabisa. Na kama nyakati hizi zinaleta kitu cho chote, hakika zinaleta na kushuhudia kweli hii.

Sasa kabla hatujaacha somo hili ninataka kujiweka wazi kabisa juu ya Ubatizo wa Roho Mtakatifu ni nini kulingana na Neno. Si kulingana na mimi, wala si kulingana na wewe. Haina budi kulingana na "Bwana asema hivi," la sivyo tunaongozwa kwa uongo. Amina.

Kwanza utaona ya kwamba katika mikutano yangu wakati nimemaliza kuhubiri huduma ya ibada ya kiinjilisti, ama ujumbe fulani wa mafundisho, ninatupa jarife na kuwaalika watu. Ninawaomba waje mbele na kumpokea Roho Mtakatifu. Marafiki zangu wa Kipentekoste, wanaponisikia nikisema jambo hili wanaamini ya kwamba ninawaalika watu waje mbele wabatizwe na Roho Mtakatifu kwa sababu tayari wamezaliwa mara ya pili. Kwa hiyo ninapowaalika wale waliojazwa Roho waje wawashughulikie wale waliojibu wito wa kumpokea Roho, hawa wapendwa husonga mbele na kuwashughulikia hao watu kana kwamba kuwatia moyo wajisalimishe kwa Mungu na waamini kunena kwa lugha. Jambo hilo limesababisha mchafuko mkubwa mno nami nataka kuwaambieni hasa yale ninayomaanisha. Ninamaanisha ya kwamba mwenye dhambi aje mbele na kuzaliwa mara ya pili, ambako ni kubatizwa katika mwili wa Kristo kwa Roho Mtakatifu ambalo ndilo hasa lililotukia pale Pentekoste wakati kanisa lilipoanzishwa. Kwa maneno mengine, kuzaliwa na Roho ni kubatizwa kwa kweli kwa Roho Mtakatifu. Ni jambo lile lile.

Sasa natambua ya kwamba litatatanisha kwa muda kidogo hapa, kwa kuwa karibu watu wote wanajua ya kwamba mimi niliwekwa wakfu kama mhubiri wa Kibatisti nami kwa uthabiti nimetangaza ya kwamba Wabatisti wamekosea kwa kusema unampokea Roho Mtakatifu WAKATI unapoamini, kwa maana hivyo sivyo. Unampokea "TANGU ulipoamini."

Matendo 19:2-6.

> *"Akawauliza, Je! Mmepokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini? Wakamjibu, La, hata kusikia kwamba kuna Roho Mtakatifu hatukusikia.*
>
> *Akawauliza, basi mlibatizwa kwa ubatizo gani? Wakasema, Kwa ubatizo wa Yohana.*
>
> *Basi Paulo akasema, Yohana kweli alibatiza kwa ubatizo wa toba, akiwaambia watu wamwamini Yeye atakayekuja nyuma yake, yaani, Kristo Yesu.*

*Waliposikia jambo hili, walibatizwa katika Jina la Bwana Yesu.*

> *Na Paulo, alipokwisha kuweka mikono yake juu yao, Roho Mtakatifu akaja juu yao; wakaanza kunena kwa lugha, na kutabiri."*

Hilo hapo. Paulo aliuliza, "Mmepokea TANGU, SI WAKATI mlipoamini." Na kuna tofauti kubwa pale, kwa maana ni BAADA ya sisi kuamini ambapo tunapokea. Efe. 1:13 ni kurudia kabisa kwa neno la yale yaliyotukia Efeso kulingana na Matendo 19,

> "Ambaye mlimwamini pia, BAADA ya kulisikia Neno la kweli, Habari Njema za wokovu wenu; Ambaye pia BAADA ya kuamini (si wakati mlipoamini) mlitiwa muhuri na Roho yule wa ahadi aliye Mtakatifu."

Sasa hili hapa neno langu. Wengi sana wa watu wetu wa kisasa na hata ndugu zetu wa kanuni (wanavyojiita) wanaamini wapate kuokolewa katika wakati fulani maalumu ambao mara nyingi unaitwa "kufanya uamuzi," na huko kumeitwa kumpokea Kristo ama kuzaliwa mara ya pili. Sasa kumpokea Kristo ni

kumpokea Roho Wake. Kumpokea Roho Wake ni kuzaliwa mara ya pili. Kumpokea Roho Wake ni kubatizwa kwa Roho Mtakatifu. Amina. Watu hawa wanaamini. Hilo ni zuri sana. Lakini wanasimama pale. Unampokea Roho Mtakatifu BAADA ya kuamini. Imekuwa hivyo daima na daima itakuwa hivyo. Neno la kwanza kabisa la kuwaelekeza watu lilikuwa ni Petro katika Pentekoste naye alisema,

> *"Tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu, katika Jina la Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu,*
>
> *Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu na kwa watoto wenu na kwa wale wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie."*

Maagizo haya yalikuja kama jibu la moja kwa moja kutoka kwa Petro kulingana na kile kilichokuwa kimetendeka Pentekoste. Kilichotimia ni kwamba Mungu kulingana na Yoeli alikuwa akimwaga Roho Mtakatifu aliyeahidiwa juu ya wote wenye mwili. Hakuwa amemwagwa kabla ya wakati huo wala kutolewa kabla ya wakati huo. Hivi ndivyo ilivyokuwa. Lakini TUKIO HILI lilikuwa lije tangu wakati wa sasa na kuendelea kwa kutubu, kubatizwa katika Jina la Bwana Yesu Kristo, na halafu Mungu alikuwa anawajibika kuwajaza wale waliokuja. Petro, wala ye yote wa hao mitume hawakusema kamwe, "Hamna budi kuzaliwa mara ya pili, kisha mjazwe na Roho."

Kwamba hicho ndicho kielelezo cha tukio kuhusiana na kumpokea Roho Mtakatifu, angalia kwa makini wakati ule hasa uliofuata ambapo Roho alishuka juu ya watu.

Matendo 8:5-17,

> *"Filipo akatelemka akaingia mji wa Samaria, akawahubiri Kristo.*
>
> *Na makutano kwa nia moja wakasikiliza maneno yale yaliyosemwa na Filipo walipoyasikia na kuziona ishara alizokuwa akizifanya.*
>
> *Kwa maana pepo wachafu wakawatoka wengi waliopagawa nao, wakilia kwa sauti kuu; na watu wengi waliopooza, na viwete, wakaponywa.*
>
> *Ikawa furaha kubwa katika mji ule.*
>
> *Lakini kulikuweko na mtu mmoja, jina lake Simoni, ambaye hapo kwanza alikuwa akifanya uchawi katika mji ule, akiwashangaza watu wa taifa la Wasamaria, akisema ya kuwa yeye ni mtu mkubwa.*
>
> *Wote wakamsikiliza tangu mdogo hata mkubwa, wakisema, Mtu huyu ni ule uweza wa Mungu, ule Mkuu.*
>
> *Wakamsikiliza, kwa maana amewashangaza muda mwingi kwa uchawi wake.*
>
> *Lakini walipomwamini Filipo, akizihubiri habari njema za ufalme wa Mungu, na Jina Lake Yesu Kristo, wakabatizwa, wanaume na wanawake.*
>
> *Na yeye Simoni mwenyewe aliamini akabatizwa, na baada ya kubatizwa akashikamana na Filipo; na akashangaa, alipoziona ishara na miujiza mikubwa inayotendeka.*
>
> *Na mitume waliokuwako Yerusalemu, waliposikia ya kwamba Samaria imelikubali Neno la Mungu, wakawapelekea Petro na Yohana;*
>
> *Ambao waliposhuka, wakawaombea wampokee Roho Mtakatifu;*
>
> *(Kwa maana bado hajawashukia hata mmoja wao, ila wamebatizwa tu kwa Jina la Bwana Yesu.)*
>
> *Ndipo wakaweka mikono yao juu yao, nao wakampokea Roho Mtakatifu.*

Kulingana na aya ya 12, WALIAMINI NENO. Wakabatizwa katika Jina la Bwana Yesu. Lakini kulingana na aya ya 16, angawa hayo yote yametendeka, walikuwa BADO HAWAKUWA WAMEMPOKEA ROHO MTAKATIFU. Ilikuwa tu ni BAADA ya kuamini na kubatizwa sawasawa ambapo walimpokea Roho Mtakatifu. Hicho ndicho kielelezo halisi kilichoandikwa katika Matendo 2:38-39.

Andiko lingine linalotupa nuru ya kustaajabisha kwenye jambo hili linapatikana katika Gal. 3:13-14,

> *"Amelaaniwa kila mtu aangikwaye juu ya mti;*
>
> *Ili kwamba baraka ya Ibrahimu iwafikilie Mataifa katika Yesu Kristo, kwamba (kusudi) tupate kupokea ahadi ya Roho kwa njia ya imani."*

Sasa kamwe haiwezi kusemwa ya kwamba "baraka ya Ibrahimu" ndiyo kuzaliwa mara ya pili, na

kwamba "ahadi ya Roho" ni Ubatizo wa Roho Mtakatifu kama matukio mawili mbalimbali. Kwa maana Maandiko yanasema hivi: "Yesu alikufa msalabani, na kwa njia ya mauti hiyo na kufufuka, baraka ya Ibrahimu iliwashukia Mataifa, ikawaacha Wayahudi. Hili lilitukia ili kwamba Roho apate kupatikana kwa Mataifa."

Ili kufahamu yale ambayo nimesema sasa hivi ni kuondoa utata kwa nini wanafunzi hawajamwona Paulo akisema wakati wo wote, "Mzaliwe mara ya pili na KISHA mjazwe na Roho." Wameliwazia liko pale, nao wameweka maana zao wenyewe kulifanya liseme hivyo, LAKINI MAANDIKO HAYASEMI JAMBO HILO. Yesu kamwe hakusema jambo hilo pia.

Angalia Yohana 7:37- 39, na uisome sasa kwa ufahamu.

> *"Hata siku ya mwisho, siku ile kubwa ya sikukuu, Yesu akasimama, akapaza sauti Yake akisema, Mtu akiona kiu, na aje Kwangu anywe.*
>
> *Aniaminiye Mimi, kama vile Maandiko yalivyonena, mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake.*
>
> *(Na Neno hilo alilisema katika habari ya ROHO, Ambaye wale wamwaminio watampokea baadaye; kwa maana Roho Mtakatifu alikuwa hajatolewa, kwa sababu Yesu alikuwa hajatukuzwa.)"*

Sasa inasema hapa dhahiri na kwa mkazo ya kwamba mwamini akinywa kwa kumjia Yesu katika imani angekuwa na mito ya maji ikitiririka kutoka kwake. Na hilo linaliweka tukio hili hapo Pentekoste.

Sasa tukiweka wazo hili akilini tunasoma Yohana 4:10 & 14,

> *"Kama ungaliijua karama ya Mungu, Naye ni nani akuambiaye, Nipe maji ninywe, ungalimwomba Yeye, Naye angalikupa maji yaliyo hai.*
>
> *Walakini ye yote atakayekunywa maji yale nitakayompa Mimi hataona kiu milele; bali yale maji nitakayompa yatakuwa ndani yake chemchemi ya maji, yakibubujikia uzima wa milele."*

Maji yaya haya yaliyo hai yametajwa, lakini wakati huu hayaitwi mto; yanaitwa chemchemi ya maji. Hapo ndipo watu wanapofanya makosa yao. Hapo ndipo watu wanapokosea. Kwa sababu yanaitwa kisima na mto, wao wanafiria ya kwamba mahali fulani ni uzima wa milele unaotolewa na Roho na katika mahali pengine ambapo yanaitwa mto (likimaanisha nguvu nyingi za kuendesha) haina budi kuwa ni Roho aliyetolewa sasa kama kipawa cha nguvu. Sivyo ilivyo. Ni kitu kile kile. Roho Ndiye anayetoa uzima na nguvu, na hilo lilikuja hapo Pentekoste.

Ni kitu gani kilichosababisha kutokufahamu huku? Jibu ni, "UJUZI". Temeongozwa na ujuzi na wala si Neno. Tupilia mbali ujuzi kama kipimo chako. Kuna timazi moja peke yake, fimbo moja tu, na hiyo ni NENO. Sasa angalia kwa makini na upate hili. Petro alisema, "Tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu katika Jina la Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi zenu nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu." Paulo alisema, "Je! Mmempokea Roho Mtakatifu Tangu mlipoamini?" Hili ndilo tatizo letu lote papa hapa. Watu wanatubu dhambi zao, wanabatizwa katika maji, LAKINI HAWAENDELEI NA KUMPOKEA ROHO MTAKATIFU. UNAAMINI HADI KUMPOKEA ROHO.

Kumwamini Yesu ni hatua nzuri ya kuelekea njia sahihi ambayo inaelelekeza kwa Roho Mtakatifu. Lakini watu wanasimama pale. Wanaenda wanafikia kwenye maji kisha wanakoma. Wanaamini, kisha wanakoma. Biblia haisemi ya kwamba unapokea WAKATI unapoamini. Swala ni, "Je! mmepokea Roho Mtakatifu TANGU mlipoamini?" Tafsiri halisi na kamili ni: "Je! ninyi zamani, mkiisha kuamini, mmempokea Roho Mtakatifu?" Watu wanaamini kisha wanakoma. Humpokei Roho Mtakatifu wakati UNAPOMWAMINI Yeye, baada ya kutubu. Unaendelea mbele na kumpokea Roho Mtakatifu. Mnaona jambo hilo? Hiyo ndiyo shida na waamini wetu wa kimsingi. Hawana nguvu kwa sababu wao wanakoma kabla ya kuifikia Pentekoste.

Wao ni kama wale wana wa Israeli waliotoka Misri na wakakoma karibu na Nchi ya Ahadi. Sasa hao wana wa Israeli walitoka Misri wakiwa karibu watu milioni mbili kamili. Walisafiri pamoja, wote waliona miujiza ya Mungu, wote walishiriki mana ile ile na maji kutoka kwenye mwamba uliopigwa, wote walilifuata wingu lile lile mchana na nguzo ya moto usiku lakini WAWILI TU ndio waliofika kwenye Nchi ya Ahadi. WAWILI TU NDIO WALIOKUWA WA KWELI AMA WAAMINI HALISI. Hiyo ni kweli kwa sababu Neno linatwambia ya kwamba hao wengine walikufa kwa sababu ya kutokuamini; na kwa sababu ya kutokuamini hawangeweza kuingia (Ebr. 3:19). Basi kwa sababu hilo ni kweli, na ni WAWILI tu ndio WALIOINGIA, basi hao wengine hawakuwa waamini wa kweli. Ni kitu gani kilicholeta tofauti? Wawili walidumu na Neno. Wakati mioyo ya wale wapelelezi wawili iliposhindwa kule Kadeshi-barnea, Yoshua na Kalebu hawakusitasita kwa maana waliamini Neno na kusema, "Sisi tunaweza hata na zaidi kuiteka hiyo nchi." Wao walijua wangeweza kwa maana Mungu alikwisha kusema, "Nimewapa hiyo nchi." Baada ya Israeli wote wale kuna nguvu na wema na ukombozi wa Mungu hawakuingia katika raha, ambao ni mfano

wa Roho Mtakatifu. Kwa hiyo unaweza kuona sasa hivi ya kwamba ni wachache sana watakaodumu kuamini hata wapate kumpokea Roho wa Mungu.

Vema, tumekuja umbali huu. Sasa nataka kusonga mbele zaidi, na nitakapofanya hivyo ninajua nitasababisha miamsho iibuke. Lakini hilo ndilo jambo ambalo siwajibiki nalo. Mimi ninawajibika kwa Mungu na Neno Lake na watu ambao Mungu amenituma kwao. Sina budi kuwa mwaminifu katika yote anayonipa kusema.

Katika Yohana 6:37 & 44 inasema,

> *"Wote anipao Baba watakuja Kwangu; wala ye yote ajaye Kwangu sitamtupa nje kamwe.*
>
> *Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba aliyenipeleka; Nami nitamfufua siku ya mwisho."*

Yohana 1:12-13,

> *"Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio Jina Lake;*
>
> *Waliozaliwa, si kwa damu, wala si kwa mapenzi ya mwili, wala si kwa mapenzi ya mtu, BALI KWA MUNGU."*

Waefeso 1:4-5,

> *"Kama vile alivyotuchagua katika Yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ili tuwe watakatifu, watu wasio na hatia mbele Zake katika pendo.*
>
> *Kwa kuwa alitangulia kutuchagua, ili tufanywe Kwake wanawe kwa njia ya Yesu Kristo, sawasawa na uradhi wa mapenzi Yake."*

Sasa bila ya kuingilia kindani sana somo la ukuu wa Mungu (kwa kuwa lenyewe lingehitaji kitabu kizima) hebu niseme hapa ya kwamba kulingana na aya hizi, Yesu Kristo anachagua bibiarusi Wake kama vile tu watu wanaume wanavyowachagua bibi-arusi wao leo. Bibi-arusi leo haamui tu kwa urahisi atamchukua mwanamume fulani kuwa mume. La bwana. Bwana arusi ndiye anayeamua na kuchagua mwanamke fulani awe bibi-arusi wake. (Yohana 15:16, "Ninyi hamkunichagua Mimi; bali mimi nimewachagua ninyi.")

Sasa kulingana na Neno la Mungu, bibi-arusi alichaguliwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Kuchaguliwa huku kwa bibi-arusi kulikusudiwa ndani Yake Mwenyewe. Waefeso 1:9.

Na katika Warumi 9:11 inasema

> *"Ili lisimame kusudi la Mungu la kuchagua."*

Huwezi kulisoma vinginevyo. Kusudi la moyoni, kusudi la milele la Mungu lilikuwa kuchukua bibi-arusi ambaye amejichagulia MWENYEWE, na kusudi hilo lilikuwa ndani Yake Mwenyewe, na kwa kuwa lilikuwa la milele lilitangazwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.

Angalia kwa makini sasa na uone jambo hili. Kabla hakujakuweko na chembe ya mavumbi ya nyota; kabla Mungu hajakuwa Mungu (Mungu ni kitu cha kuabudiwa na kapakuwepo na mtu wa kumwabudu Yeye, kwa hiyo Yeye wakati huo alikuwa Mungu kwa uwezekano.) Naye alijulikana tu kama Roho wa milele, bibi arusi alikuwa tayari niani Mwake Naam, alikuwa. Alikuwa akiishi katika mawazo Yake. Na vipi kuhusu mawazo hayo ya Mungu? Hayo ni ya milele, sivyo?

Mawazo ya milele ya Mungu! Hebu niwaulize, "Je! Mawazo ya Mungu ni ya milele?" Kama unaweza kuona jambo hili, utaona mambo mengi. Mungu habadiliki katika asili na tabia. Tumejifunza hilo na kuthibitisha hilo tayari. Mungu hana kikomo katika uweza wake kwa hiyo Yeye kama Mungu hana budi kuwa anayejua yote. Kama Yeye ni ajuaye yote, basi Yeye sasa hajifunzi, wala hata hajishauri Mwenyewe, wala wakati wo wote haongezei kwenye maarifa Yake. Kama anaweza kuongeza kwenye maarifa Yake, basi Yeye hajui yote. Sana sana tunaloweza kusema ni kwamba atakuwa hivyo wakati fulani. Lakini hilo si la Kimaandiko.

Yeye NI anayejua yote. Yeye hajawahi kuwa na wazo jipya juu ya jambo lo lote kwa maana mawazo Yake yote amekuwa nayo daima na atakuwa nayo daima, na anajua mwisho kutoka mwanzo kwa sababu Yeye ni Mungu. KWA HIYO MAWAZO YA MUNGU NI YA MILELE. NI HALISI. Hayo si kama tu mtu mwenye kielelezo alichochora na ambacho siku moja kitageuzwa kuwa kitu kinachoonekana na chenye umbo, lakini hayo ni halisi tayari na ni ya milele, na ni sehemu ya Mungu.

Angalia jinsi jambo hili linavyofanya kazi. Mungu daima alikuwa na mawazo yake kuhusiana na Adamu. Adamu, kama mawazo Yake, alikuwa bado hajadhihirishwa.

Zaburi 139:15-16 itawapa wazo kidogo juu ya jambo hili,

*"Mifupa yangu haikusitirika Kwako, nlipoumbwa kwa siri, nilipoungwa kwa ustadi pande za chini za nchi;*

*Macho Yako yaliniona kabla sijakamilika; chuoni Mwako ziliandikwa zote pia, siku zilizoamriwa kabla hazijawa bado."*

Hilo, kama nilivyosema, halikuandikwa juu ya Adamu lakini linakupa fununu na ujuzi kwamba wazo lilikuwepo katika nia Yake, na wazo hilo lilikuwa la milele na lilipaswa kudhihirishwa. Kwa hiyo wakati Adamu alipofanywa kwa mavumbi ya ardhi na utu wake wa kiroho ukaumbwa na Mungu, basi Adamu akawa wazo la Mungu lililodhihirishwa, na mawazo hayo ya milele yalidhihirishwa sasa.

Tungeweza kushuka kupitia katika karne nyingi. Tunawaona akina Musa, akina Yeremia, akina Yohana Mbatizaji, na kila mmoja wa hawa alikuwa wazo la Mungu la milele lililodhihirishwa katika majira yake. Halafu tunakuja kwa Yesu aliye LOGOS. Yeye alikuwa lile WAZO timilifu na kamilifu lililodhihirishwa na Yeye akajulikana kama Neno. Hivyo ndivyo ALIVYO, na milele ATAKUWA.

Sasa inasema ya kwamba "Ametuchagua KATIKA YEYE (Yesu) kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu." Hilo linamaanisha tulikuweko PAMOJA Naye papo hapo katika nia na mawazo ya Mungu kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Hiyo inawapa wateule sifa ya Milele. Huwezi kuepuka jambo hilo.

Hebu niingize wazo hapa ndani. Hata kuzaliwa kwetu kwa kawaida kunategemea kuchaguliwa. Vifuko vya mayai huzaa mayai mengi, mengi sana. Lakini ni kwa nini kwamba kwa wakati fulani yai fulani hushuka na wala si lingine? Na halafu kati ya mbegu za mwanamume, kwa sababu isiyojulikana chembechembe fulani hujishikiza kwenye yai wakati nyingine ambazo zingaliweza tu kujishikiza kwa urahisi, ama zilikuwa na nafasi nzuri ya kufanya jambo hilo hazikufanya hivyo na zikafa. Kuna kichwa fulani nyuma ya yote haya, kama sivyo ni kitu gani kinachoamua kama mtoto fulani ni mvulana au msichana, ana nywele za shaba ama nyeusi, macho maangavu ama meusi, nk. Tukiwa na mawazo haya kwenye mioyo na tuwazie juu ya Yoshua na Kalebu.

Je! Yesu hakusema katika Yohana 6:49

*"Baba zenu waliila mana jangwani; wakafa?"*

Hao wazazi waliokufa walikuwa muhimu kama mababu wa watu ambao Yesu alikuwa akinena nao. Waliangamia, hata hivyo walikuwa katika uchaguzi wa Mungu kimwili kama vile Yoshua na Kalebu wlivyokuwa Kiroho.

Lakini kwa kuendelea. Wateule hawa hawakuwa mawazo ya milele ya Mungu ambayo yalikuwa yadhihirishwe katika mwili katika majira yao, lakini wateule wawa hawa wanaitwa kwa jina lingine.

Warumi 4:16.

*"Kwa hiyo ilitoka katika imani, iwe kwa njia ya neema, ili kwamba ile ahadi iwe imara kwa wazao wote; si kwa wale wa torati tu, ila na kwa wale wa imani ya Ibrahimu; aliye baba yetu sisi sote."*

Warumi 9:7-13,

*"Wala hawawi wote wana kwa kuwa wazao wa Ibrahimu, bali, Katika Isaka wazao wako wataitwa.*

*Yaani, si watoto wa mwili walio watoto wa Mungu, bali watoto wa ile ahadi wanahesabiwa kuwa wazao.*

*Kwa maana neno la ahadi ni hili, Panapo wakati huu nitakuja, na Sara atakuwa na Mwana.*

*Wala si hivyo tu, lakini Rebeka naye, akiisha kuchukua mimba kwa mume mmoja, naye ni Isaka, baba yetu,*

*(Kwa maana kabla hawajazaliwa wale watoto, wala hawajatenda neno jema wala baya, ili lisimame kusudi la Mungu la kuchagua, si kwa sababu ya matendo, bali kwa sababu ya nia Yake aitaye;)*

*Aliambiwa hivi, Mkubwa atamtumikia mdogo.*

*Kama ilivyoandikwa, Nimempenda Yakobo, bali Esau nimemchukia."*

Wagalatia 3:16,

*"Basi ahadi zilinenwa kwa Ibrahimu na kwa mzao wake. Hasemi, Kwa wazao, kana*

*kwamba ni wengi, bali kana kwamba ni mmoja, Kwa mzao wako, yaani, Kristo."*

Wagalatia 3:29,

*"Na kama ninyi ni wa Kristo, basi, mmekuwa uzao wa Ibrahimu, na warithi sawaswa na ahadi."*

Kulingana na Rum. 4:16 tunaona ya kwamba Mungu ametoa Ahadi ya Hakika kwa uzao WOTE wa Ibrahimu, na Paulo anajiweka mwenyewe pamoja na waamini wote chini ya kundi hilo kwa sababu anasema "Ibrahimu aliye baba yetu sisi SOTE." Ndipo anaendelea si kupunguza tu maelezo yake, lakini kuyatimiliza kwa kuwa katika Gal 3 yeye anautambulisha yule MZAO (umoja) na Yesu, na kuwahesabu "watoto walio ule uzao" kama watoto wa ahadi, na ahadi kana kwamba ina uhusiano na "kuchaguliwa", ama "uchaguzi wa Mungu." Na hilo ndilo tumekuwa tukisema hasa. Hawa walio wa Uzao wa Kifalme ndio wateule wa Mungu; ndio wamechaguliwa tangu zamani, walikwisha kujulikana na Mungu tangu zamani, nao walikuwa katika nia ya Mungu na katika mawazo Yake.

Katika lugha dhahiri sana Bibi-arusi wa Kweli wa Kristo alikuwa katika nia ya Mungu milele, ingawa hakuwa amedhihirishwa mpaka kila mmoja wao alipojitokeza katika majira yaliyokusudiwa, yaliyoamriwa. Wakati kila mshiriki alipokuwa anatokea ALIDHIHIRISHWA na kupachukua mahali pake katika ule mwili. Hivyo basi bibi-arusi huyu ni BIBI-ARUSI halisi WA UZAO WA NENO LILILONENWA. Na ingawa yeye anatajwa kama mwanamke yeye pia anaitwa "mwili wa Kristo." Ni wazi sana ya kwamba anapaswa kuitwa hivyo kwa kuwa yeye alichaguliwa tangu zamani katika Yeye, alitoka kwenye schanzo kile kile, alikuwa pamoja Naye milele, na sasa anamdhihirisha Mungu katika mwili wenye washiriki wengi ambapo Mungu wakati mmoja alidhihirishwa katika MSHIRIKI MMOJA, yaani Bwana wetu Yesu Kristo.

Sasa basi, hapa tunafikia neno la mwisho. *Kama vile Logos (Mungu) wa milele alivyodhihirishwa katika Mwana, na katika Yesu mlikaa utimilifu wote wa Uungu kwa jinsi ya mwili, na Yule wa Milele alikuwa ni yule Baba aliyedhihirishwa katika mwili, na hapo akapata sifa ya Mwana, vivyo hivyo sisi, tukiwa wa milele katika mawazo Yake nasi tulifanyika Uzao wa washiriki wengi wa Neno Lililonenwa, waliodhihirishwa katika mwili, na hayo mawazo ya milele sasa yaliyodhihirishwa katika mwili sasa ni wana wa Mungu, kama vile sisi tunavyoitwa.* HATUKUFANYIKA UZAO KWA KUZALIWA MARA YA PILI, SISI TULIKUWA NI UZAO NA KWA HIYO TUKAZALIWA MARA YA PILI KWA KUWA WATEULE TU NDIO WANAOWEZA KUZALIWA MARA YA PILI. Kwa sababu TULIKUWA UZAO ndiyo sababu tumeweza kuhuishwa. Kwa WASIO UZAO hakuna kitu cha kuhuisha.

Shikilia jambo hili kwa makini moyoni. Sasa chukua hatua inayofuatia. Kukomboa maana yake ni kununua tena. Kunarudisha kwa Mwenyewe wa asili. Mungu, kwa mauti Yake, ile damu iliyomwagika ILINUNUA KUWARUDISHA WALIO WAKE. Yeye alimnunua na kumrudisha Bibi-arusi Mbegu aliye Neno Lililonenwa. "Kondoo wangu wanaisikia sauti Yangu (Neno) nao wananifuata Mimi." Wewe daima ulikuwa kondoo. Kamwe hukuwa nguruwe wala mbwa aliyegeuzwa kuwa kondoo. Hilo haliwezekani kwa maana kila aina ya uhai huzaa wa jinsi yake wala hakuna mabadiliko katika jamii. Kama vile tulivyokuwa katika mawazo ya Mungu kisha tukadhihirishwa katika mwili, ilibidi siku ije ambapo tungeisikia sauti Yake (Neno), na kwa kusikia sauti hiyo tutambue Baba yetu anatuita, na tutambue ya kwamba sisi ni wana wa Mungu. Tuliisikia sauti Yake na tukalia kama vile mwana mpotevu, "Niokoe, Ee, Baba yangu. Ninarudi Kwako."

Mwana wa Mungu anaweza kwenda wakati mrefu kabla ya kutambua ya kwamba yeye ni mwana. Kwa kweli Wakristo wengi wa kweli ni kama ile hadithi ya yule kifaranga wa tai aliyeanguliwa chini ya kuku. Unajua ya kwamba tai ni mfano wa mwamini wa kweli. Vema, mkulima alitwaa yai kutoka kwenye kiota cha tai na kuliweka chini ya kuku. Wakati ulipotimia mayai yote yaliyokuwa chini ya yule kuku yakaanguliwa. Vifaranga vya kuku viliendelea vizuri na mama kuku lakini maskini tai huyo mdogo hakuweza kuuelewa ule mlio na kule kukwaruza-kwaruza kwa ajili ya kupata chakula kwenye lile lundo la samadi. Alifaulu kupata riziki walakini alichanganyikiwa sana juu ya jambo hilo lote.

Lakini siku moja, kutoka mbali huko juu mbali hewani yule mama tai aliyekuwa amelitaga lile yai alimwona huyo tai mdogo ardhini. Akashuka chini kwa kasi sana na kumpigia makelele kwa sauti yake yote ili aruke aje kukutana naye. Hakuwa kamwe amesikia mlio wa tai, lakini wakati aliposikia mlio huo wa kwanza kitu fulani ndani yake kilichochewa naye akatamani kuruka auendee. Lakini aliogopa kujaribu. Tena mama huyo akampigia makelele kwamba aruke hewani amfuate. Akajibu kwa sauti kuu ya hofu ya kwamba alikuwa anaogopa. Mara nyingine tena akaita, akilia kwa sauti kuu kwamba ajaribu. Huku anapigapiga mabawa yake alijitupa kwa nguvu hewani, na akijibu mlio wa mamaye, alipaa angani kwenye mbingu za samawati. Mnaona yeye daima alikuwa tai. Alitenda kama kuku kwa muda kidogo lakini hakuweza kuridhika. Lakini aliposikia wito wa yule tai mkuu alifika mahali pake mwenyewe. Na mara mwana wa kweli wa Mungu anaposikia kilio cha Roho kwa Neno, yeye pia, atajitambua yeye yu nani na kukimbilia kwa Nabii Mkuu Tai na kuwa pamoja Naye milele ameketi katika ulimwengu wa roho katika Kristo Yesu.

SASA LAJA JIWE LETU LA USHINDI LA KIFUNIKO juu ya ubatizo wa Roho Mtakatifu.

Wagalatia 4:4-7,

*"Hata ulipowadia utimilifu wa wakati, Mungu alimtuma Mwanawe ambaye amezaliwa na mwanamke, amezaliwa chini ya sheria,*

*Kusudi awakomboe hao waliokuwa chini ya sheria, ili sisi tupate kupokea hali ya kuwa wana.*

*Na kwa kuwa ninyi mmekuwa wana, Mungu alimtuma Roho wa Mwanawe mioyoni mwenu, aliaye, Aba, yaani, Baba.*

*Kama ni hivyo, wewe si mtumwa tena bali u mwana; na kama u mwana, basi, u mrithi kwa Mungu kwa njia ya Kristo."*

Hilo hapo. Yesu Kristo alikuja, akafa msalabani, na akatimiza Ukombozi (akiturudisha kwa Mwenyewe wa asili kwa njia ya kutununua, ama kulipa deni) na hapo AKATUWEKA KAMA WANA. Yeye hakutufanya wana, kwa kuwa tayari tulikuwa wanawe, lakini alituweka kama wana; kwa kuwa mradi tu tulikuwa ulimwenguni, katika mwili, hatungeweza kutambuliwa kama wanawe. Tulishikwa mateka na Ibilisi. Lakini tulikuwa wana, hata hivyo. Basi sikilizeni jambo hili: NA KWA KUWA NINYI NI WANA, MUNGU ALIMTUMA ROHO WA MWANAWE MIOYONI MWENU, AMBAYE KWA HUYO MNALIA, BABA, BABA." Roho alishuka juu ya nani pale Pentekoste? Wana. Huko Korintho? Juu ya Wana wakati walipolisikia NENO.

Ubatizo wa Roho Mtakatifu ni nini? Ni Roho akikubatiza katika ule mwili wa Kristo. Ni kuzaliwa upya. Ni Roho wa Mungu akiingia na kukujaza ukiisha kutubu, (ukiisha kulisikia Neno Lake) na kwisha kubatizwa katika maji kama jibu la dhamiri njema kwa Mungu.

Yale tuliyokwisha kueleza sasa hivi yangekuwa rahisi zaidi kwa watu wote kuelewa kama wote wangeliamini fundisho la umoja wa Uungu. Kwa kuwa hakuna nafsi tatu katika Uungu ule ila MOJA. Hivyo HATUZALIWI mara ya pili kwa Roho wa uzima wa Yesu akiingia ndani, na halafu baadaye Roho Mtakatifu anaingia kutupa nguvu. Kama hilo lingalikuwa ni kweli, mbona tunashindwa kumheshimu Baba kwa kutokumpa Yeye sehemu fulani katika ukombozi wetu mkamilifu, kwa maana kama wokovu ni wa Bwana na kuna Bwana watatu, basi YEYE (Baba) hana budi kuwa na jambo la kufanya, pia. Lakini hakika inaweza kuonekana ya kwamba Yesu alifanya jambo hili dhahiri sana ya kwamba ilikuwa ni Yeye na Yeye peke yake Aliye Mungu na ni Yeye na Yeye peke yake Ambaye anaingia ndani ya mwamini.

Yohana 14:16 inasema ya kwamba Baba atamtuma Mfariji mwingine.

Lakini aya ya 17 inasema ya kwamba Yeye (Yesu) anakaa pamoja nao na anapaswa kuwa ndani yao baadaye.

Katika kifungu cha 18 Yeye anasema atawajia.

Katika aya ya 23 katika kuzungumza na wanafunzi Yeye alisema, "Sisi (Baba na Mwana) tutakuja kwake." Kwa hiyo ni Baba, Mwana na Roho Mtakatifu wote wakija kwa wakati mmoja kwa maana Uungu NI MTU MMOJA. Kuja huko kulitukia pale Pentekoste. Hakuna kuja kuwili kwa Roho, ni kumoja tu. Shida ni kwamba watu hawajui ukweli halisi, nao wanamwamini Yesu tu kwa ajili ya ondoleo la dhambi lakini hawasongi mbele kamwe wakampokee Roho.

Kabla sijafunga somo hili, najua kuna swali mioyoni mwenu. Mtataka kujua kama ninaamini katika fundisho la mtu kuishi kabla ya kuzaliwa. Mimi siamini katika fundisho hilo la Kimormoni la kuweko kwa nafsi kabla mtu kuzaliwa zaidi ya ninavyoamini katika kufanyika mtu tena ama roho ya mtu kuingia katika mwili mwingine mtu afapo. Uwe mwangalifu hapa na uone jambo hili. Si mtu anayekuja aliyechaguliwa tangu zamani na Mungu, NI NENO, AMA UZAO. Hivyo ndivyo ilivyo. Huko nyuma kabisa, huko nyuma zamani sana hata akili za mwanadamu haziwezi kufahamu, Mungu wa Milele pamoja na mawazo ya milele, aliwaza na kutangaza,

"NIMEMPENDA YAKOBO, BALI ESAU NIMEMCHUKIA,

(Warumi 9:13)

WALA HAWAJAZALIWA, WALA HAWAJATENDA NENO JEMA WALA BAYA."

Mnaona, ilikuwa ni WAZO, na halafu hilo wazo likadhihirishwa, na Mungu akamkomboa Yakobo, kwa maana Yakobo ndiye pekee aliyekuwa MZAO; Yakobo, ndiye peke yake aliyekuwa mzao; hiyo ndiyo sababu aliiheshimu ile haki ya mzaliwa wa kwanza na agano la Mungu. Kama wewe ni mzao wa kweli, utalisikia hilo Neno; Roho atakubatiza katika mwili wa Kristo, akikujaza na kukutia nguvu, nawe utalipokea Neno la siku yako na wakati wako. Mnaona jinsi ushuhuda wa kweli unavyokuwa wakati Neno linapofunuliwa kwako? Tena, angalia, Yesu alikuwa Uzao wa Kifalme. Yeye aliishi katika mwili wa mwanadamu. Wakati Roho alipomwita (Wazo Lililodhihirishwa kwa Neno), alienda Yordani na akabatizwa kule ndani ya maji. Baada ya kulitii Neno, Roho Mtakatifu alishuka juu Yake na sauti ikasema, "Huyu ni

Mwanangu mpendwa Wangu, msikieni Yeye.” Hiyo sauti haikusema, “Huyu amekuwa Mwanangu,” Yesu ALIKUWA ndiye huyo Mwana. Roho Mtakatifu alimweka mahali Pake kama huyo Mwana mbele yao wote. Ndipo baada ya kujazwa namna hiyo (na kielelezo hicho hicho kinatumika pale Pentekoste na daima baadaye), alienda zake katika onyesho la nguvu, akipokea ufunuo mkamilifu wa Mungu na kutoka kwa Mungu, kwa ajili ya siku hiyo.

Sasa tumekuwa daima tukisema ya kwamba ushuhuda wa kweli wa kubatizwa na Roho Mtakatifu ni kwa mwamini kulipokea Neno kwa wakati anaoishi. Hebu niwaonyesheni wazi wazi kabisa.

Zile Nyakati Saba kama zilivyoelezewa katika Ufu. Sura ya 2 & 3 zinachukua wakati wote mzima wa Utimilifu wa Mataifa, ama wakati wote ambao Mungu anawashughulikia Mataifa katika wokovu. Katika kila wakati, bila kuondoa mmojawapo, inasema jambo lile lile katika kufungua na kufunga ujumbe wa kila wakati. “Kwa mjumbe wa (Efeso, Smirna, Pergamo, Thiatira, Sardi, Filadelfia, Laodikia) andika; Haya ndiyo asemayo Yeye, nk., nk. ”... Yeye aliye na sikio, na alisikie (umoja) Neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa.“ Angalia hapa ya kwamba Yesu (kwa Roho) katika KILA wakati anamwandikia mtu MMOJA TU kuhusiana na Neno la wakati huo. Ni mjumbe MMOJA tu kwa kila wakati anayepokea yale Roho anayouambia wakati huo, na MJUMBE HUYO MMOJA ndiye mjumbe wa kanisa la kweli. Yeye anazungumza kwa niaba ya Mungu kwa ufunuo kwa ”makanisa“, yote mawili la kweli na la uongo. Ujumbe huo ndipo unatangazwa kwa wote. Lakini ingawa unatangazwa kwa ajili ya wote wanaokuja katika eneo la huo ujumbe, ujumbe huo unapokelewa kibinafsi na kundi fulani pekee linalostahili kwa njia fulani. Kila mtu binafsi wa kundi hilo ni yule aliye na uwezo wa kusikia yale Roho anayosema kwa njia ya mjumbe huyo. Wale wanaosikia hawapati ufunuo wao wa kipekee, wala kundi fulani halipati ufunuo wao wa pamoja, BALI KILA MTU ANASIKIA NA KUPOKEA AMBAYO HUYO MJUMBE AMEISHAPOKEA TAYARI KUTOKA KWA MUNGU.

Sasa usifikirie ni ajabu ya kwamba hivi ndivyo ilivyo, kwa maana Paulo aliweka kielelezo hiki chini ya mkono wa Mungu. Paulo ndiye peke yake aliyekuwa na ufunuo kamili kwa ajili ya siku yake kama inavyothibitishwa na kukabiliana kwake na wale mitume wengine waliokubali kwamba Paulo alikuwa ndiye Nabii-Mjumbe kwa Mataifa kwa ajili ya siku hiyo. Na pia angalia kwa ule mfano halisi katika Neno, ya kwamba wakati Paulo alipotaka kwenda Asia, Mungu alimkataza, kwa maana kondoo (watoto Wake) walikuwa Makedonia nao (hao Wamakedonia) wangesikia yale ambayo Roho aangesema kupitia kwa Paulo, wakati watu wa Asia hawangesikia.

Katika kila wakati tuna kielelezo cha namna ile ile. Hiyo ndiyo sababu nuru huja kupitia kwa mjumbe fulani aliyetolewa na Mungu katika eneo fulani, halafu kutoka kwa mjumbe huyo nuru inaenea kwa kupitia huduma ya wengine ambao wamefundishwa kwa uaminifu. Lakini bila shaka hao wote wanaotoka daima hawajifunzi jinsi ilivyo muhimu kusema yale TU yule mjumbe aliyosema. (Kumbukeni, Paulo aliwaonya watu waseme tu yale aliyosema, I Wakorintho 14:37, “*Mtu akijiona ya kwamba yeye ni nabii au mtu wa rohoni, na ayatambue hayo ninayowaandikia, ya kwamba ni MAAGIZO YA BWANA. Au je! Neno la Mungu lilitoka kwenu, au kuwafikia ninyipeke yenu?”*) Wao wanaongeza hapa, ama wanaondoa pale, na mara ujumbe si safi tena, na uamsho unakufa. Jinsi tunavyopaswa kuwa waangalifu kusikia sauti MOJA, kwa maana Roho hana ila sauti moja ambayo ni sauti ya Mungu. Paulo aliwaonya waseme yale aliyosema, yaani kama vile Petro alivyofanya vivyo hivyo. Aliwaonya ya kwamba HATA YEYE (PAULO) asingeweza kubadilisha hata neno moja la yale aliyokuwa ametoa kwa ufunuo. Loo, jinsi ilivyo muhimu kuisikia sauti ya Mungu kwa njia ya wajumbe Wake, na kisha kusema yale waliyopewa kuyaambia makanisa.

Natumaini mnaanza kuliona sasa. Labda mnaweza kuelewa sasa ni kwa nini sikubaliani na wale wa kimsingi na Wapentekoste. Sina budi kushikilia Neno jinsi ile Bwana alivyolifunua. Sasa sikumaliza kila kitu. Hilo lingehitaji kitabu kingine kando, lakini kwa msaada wa Bwana tutapata mahubiri mengi na kanda na jumbe juu ya mambo haya yote kuwasaidia mfahamu na kuyaunganisha Maandiko yote pamoja.

*“Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa ya kila wakati.”* Katika kila wakati kilio kilikuwa ni kile kile. Sikia yale Roho asemayo. Kama wewe ni Mkristo, utarudi kwenye yale Roho anayofundisha, hiyo ni kusema, Neno la wakati huu. Kila mjumbe kwa kila wakati atahubiri Neno hilo. Kila uamsho mpya na wa kweli utatokea kwa sababu watu wamerudi kwenye Neno la wakati wao. Kilio cha kila wakati ni onyo, “Mmeliacha Neno la Mungu. Tubuni, na mlirudie Neno.” Kutoka kwenye kitabu cha kwanza katika Biblia (Mwanzo) hadi kitabu cha mwisho (Ufunuo) kuna sababu moja tu ya ghadhabu ya Mungu—kuliacha Neno; na kuna dawa moja tu ya kupata tena upendeleo Wake—kurudi kwenye Neno.

Katika Wakati wa Efeso, na katika wakati huu, na katika kila wakati tutakaofikiria tutaona ya kwamba jambo hili ni kweli. Na katika wakati wa mwisho ambao ni wakati wetu, tutaona kutiwa giza kwa Neno, ule ukengeufu mkamilifu ukiishia kwenye ile dhiki kuu.

Kama wewe ni uzao wa kweli, kama kweli umebatizwa na Roho Mtakatifu utaliheshimu Neno Lake kuliko riziki yako ya lazima, na kutamani kuishi kwa KILA Neno linalotoka katika kinywa cha Mungu.

Haya ndiyo maombi yangu ya bidii kwa ajili yetu sote; hebu tusikie yale ambayo Roho anatuletea kutoka kwenye Neno leo.

MESSAGE hub online
www.messagehub.info

Mahubiri Na
William Marrion Branham
"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7